# Nipashe
Jumapili Desemba 3, 2023 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • No. 0581513

www.ippmedia.com

JUMAPILI

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper LIKE & FOLLOW US


UKURASA 2

**Askofu** Kweka atakumbukwa kwa kazi hizi



UKURASA 4

**Atamani** wabunge walipwe mishahara 700,000/- kwa mwezi

UKURASA 5



**Aliyehitimu** udaktari na umri mdogo atoboa siri



**RONALDO AKEJELIWA KWA JINA LA MESSI**

UKURASA 21



# SERIKALI YAVUNJA UKIMYA KUHUSU MAKAMU WA RAIS

• **Yabainisha** mahali aliko, anafanya nini... *Endelea Ukurasa 2*

## Polisi yakiri ni chanzo kuchelewa uchunguzi maabara

UKURASA 3



Rais Samia Suluhu Hassan akifurahia jambo na Rais wa Afrika Kusini, Cyril Ramaphosa (kulia) pamoja na Rais wa Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), Dk. Akinumwi Adesina, baada ya kuzindua mradi wa nishati safi ya kupikia itakayowasaidia wanawake barani Afrika (AWCCSP), katika mkutano uliofanyika Dubai, Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE) jana. **PICHA: IKULU**



VITA UKEKETAJI

## Mangariba wabadili mbinu kukwepa mkono wa sheria

UKURASA 4

MICHEZO **USALAMA WA DIAMOND MASHAKANI?** UK.20 **MAONI, KATUNI** UK.6

# Askofu Kweka atakumbukwa kwa mambo haya

**Na Godfrey Mushi,** HAI

ASKOFU Mstaafu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Dayosisi ya Kaskazini, Dk. Erasto Kweka (89), ameacha alama ya kukumbukwa ndani na nje ya kanisa kutokana na mambo mbalimbali aliyoyafanya wakati wa uongozi wake.

Askofu Dk. Kweka, aliyefariki dunia Novemba 25, mwaka huu, katika Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI) akipatiwa matibabu, ndiye kiongozi aliyeanzisha Shirika la Watawa la Usharika wa Neema kabla ya kuingizwa katika baadhi ya dayosisi na baadhi zimeanzisha mpango wa kuwa na watu hao.

Mkuu wa KKKT, Askofu Dk. Frederick Shoo, akizungumza katika mahojiano maalum na Nipashe juzi, alisema alama alizoacha Dk. Kweka, mojawapo ni utashi wake wa kuanzishwa shirika hilo kitu ambacho hakikuwahi kudhaniwa ndani ya kanisa.

Watawa hao wanaoishi nje kidogo ya Hospitali ya Rufani ya Kanda ya KCMC, licha ya kufanya kazi za kikuhani, wana haiba ile ile kama ya watawa wa Kanisa Katoliki nchini.

Askofu Dk. Kweka aliyehudumu nafasi ya Askofu wa Dayosisi hiyo kwa miaka 28, baada ya kufariki dunia aliyekuwa Mkuu wa Kwanza wa KKKT, Dk. Stephano Moshi, atakumbukwa pia kwa kuanzishwa Chuo Kikuu Kushiriki cha Sayansi ya Tiba cha KCMCo.

Aidha, wakati akihudumu kama Askofu, ndiye aliyeliongoza KKKT kuridhia kupandisha hadhi Hospitali ya KCMC kuwa Hospitali ya Rufani.

Pia atakumbukwa kama mbeba maono na mwanzilishi wa Chama cha Ushirika wa Akiba na Mikopo cha ELCT-ND 1994, ambacho kinashika nafasi ya tatu kwa ukubwa wa mitaji nchini kikiwa na zaidi ya Sh. bilioni 10.

Katika huduma za kijamii, Askofu Kweka alishiriki katika uanzishwaji wa hospitali, vituo vya afya, zahanati, shule na vyuo vya ufundi. Huduma hizo zimetoa mchango mkubwa katika masuala ya afya na elimu.

Enzi za uhai wake, Askofu Dk. Kweka alibarikiwa kuwa Mchungaji mwaka 1965 kabla ya kuwa Msaidizi wa Askofu Dk. Moshi ambaye alikuwa Mkuu wa Kwanza wa Dayosisi ya Kaskazini.

Alichaguliwa kuwa Askofu wa pili wa Dayosisi mwaka 1977 akipokea kijiti hicho kwa Dk. Moshi na kuhudumu katika wadhifa huo hadi mwaka 2004 alipochaguliwa Askofu Dk. Martin Shao, kumrithi.

Kwa mujibu wa Askofu wa Dk.Shoo, mwili wa Askofu Dk.Kweka utazikwa nyumbani kwake Kijiji cha Uswaa, Wilaya ya Hai, mkoani Kilimanjaro, Desemba 6, mwaka huu.

# Serikali yavunja ukimya kuhusu Dk. Mpango

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amesema Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, yuko nje ya nchi kikazi na kuwataka Watanzania kupuuza taarifa zinazoenezwa katika mitandao ya kijamii.

Majaliwa alisema hayo jana katika ukumbi wa Halmashauri ya Jiji la Dodoma uliokoo Mji wa Serikali, Mtumba, wakati akizungumza na washiriki na wadau mbalimbali kwenye kilele cha maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Watu Wenye Ulemavu Duniani.

"Mweshimiwa Rais, Dk. Samia Suluhu Hassan, anawasalimu sana na Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, pia anawasalimu sana kwa kuwa yupo nje ya nchi ana majukumu. Acheni kusikiliza zile taarifa zinazotolewa kwenye mitandao ambazo nimeziona hivi sasa," alisema Majaliwa.

Kuhusu maadhimisho hayo, alisema serikali imeanza ujenzi wa vyuo vipya vitatu vya ufundi stadi na marekebisho kwa watu wenye ulemavu katika mikoa ya Ruvuma, Kigoma na Songwe ili kusogeza huduma hii karibu na wananchi.

"Mradi huu katika mwaka wa fedha 2022/2023 ulitengewa Sh. bilioni tatu na katika mwaka 2023/2024 umetengewa Sh. bilioni tatu nyingine. Tayari miundombinu ya madarasa, mabweni, nyumba za watumishi na ofisi za walimu zimeanza kujengwa sambamba na karakana ambazo hazihitaji majengo maalum," alisema.

Majaliwa alisema serikali imetoa Sh. milioni 960 kwa ajili ya ujenzi wa mabweni tisa kwenye shule nane zenye wanafunzi wenye mahitaji maalum katika mikoa ya Shinyanga (Shule ya Buhangija); Njombe (Shule ya Idofi) na Arusha (Shule ya Longido).

Pia alitaja mikoa mingine ni Lindi (Shule ya Mtanga); Tabora (Shule ya Goweko); Singida (Shule ya Darajani); Manyara (Shule ya Songambele) na Rukwa (Shule ya Msanzi).

"Kama mtakumbuka, fedha hizo zilitengwa kwa ajili ya sherehe za miaka 61 ya Uhuru mnamo Desemba, 2022, lakini Mheshimiwa Rais wetu kwa mapenzi makubwa alielekeza zikajenge miundombinu ya shule hizo," alisema.

Kuhusu kuimarisha upatikanaji wa miundombinu ya elimu, Waziri Mkuu alisema serikali inaendelea kumalizia ujenzi wa shule maalum ya Mbuye iliyoko Chato, mkoani Geita yenye "blocks" tatu ikiwamo awali, msingi na sekondari ya chini na juu ambayo imekamilika kwa asilimia 95 na ina uwezo wa kuchukua wanafunzi 1,200.

Akizungumzia maboresho ya utoaji wa huduma za afya, Majaliwa alisema katika kipindi cha mwaka 2022/2023, serikali imetoa huduma za afya kwa makundi maalumu kwa msamaha katika vituo vya kutolea ambapo jumla ya wahitaji 5,225,761 walipatiwa huduma kwa msamaha wakiwamo watu wenye ulemavu, na huduma hizo zimegharimu Sh. bilioni 570.67.

Katika hatua nyingine, Waziri Mkuu ameiagiza Wizara ya Uchukuzi ihakikishe kuwa kila palipo na makutano ya reli na barabara pawekwe taa za kuashiria au kifungio cha automatiki cha kuzuia na kuruhusu magari ili kunusuru maisha ya Watanzania.



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Zanzibar, Jamal Kassim Ally (kushoto), akikabidhi tuzo kwa Mkurugenzi Mkuu wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF), Hosea Kashimba, jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. Baada ya PSSSF kuibuka mshindi wa kwanza wa tuzo ya umahiri katika uandaaji wa taarifa za mahesabu kwa mwaka unaoishia 2022, zilizoandaliwa na Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu Tanzania (NBAA). **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# PSSSF yatwaa tuzo umahiri taarifa za fedha

**Na Mwandishi Wetu**

MFUKO wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF) umetunukiwa tuzo ya mshindi wa kwanza ya umahiri katika uandaaji wa taarifa za fedha kwa mwaka unaoishia 2022.

Ushindi huo ni katika kundi la hifadhi ya jamii.

Utoaji wa tuzo ulioratibiwa na Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu (NBAA) ulifanyika juzi Dar es Salaam na washindi katika makundi mbalimbali walikabidhiwa tuzo zao na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Zanzibar, CPA Jamal Kassim Ally.

Tuzo hiyo ilipokewa na Mkurugenzi Mkuu wake, CPA Hosea Kashimba ambaye aliongozana na baadhi ya watumishi kutoka Kurugenzi ya Fedha wakiongozwa na mkurugenzi wake, Beatrice Lupi.

"Kwa kweli tunamshukuru Mungu kwa tuzo hii kwani hii mara ya pili kupata tuzo hii na ni wazi kwamba watumishi wetu wanafanya kazi kwa umahiri wa hali ya juu sana. Hakika nawapongeza na nawaomba waendelee kufanya kazi kwa kuzingatia ubora na taratabu zote za ndani na za kimataifa," alisema.

Kashimba alisema lengo la PSSSF siku zote ni kuishi dira yake ambayo ni kuwa mfuko unatoa huduma bora zaidi za hifadhi ya jamii nchini na ili lengo hilo lifikiwe, mfuko unatumia wafanyakazi wenye uwezo, ari na kutumia teknolojia ya kisasa.

"Sisi PSSSF tuna maadili yetu ambayo ninaamini ndiyo chachu ya kufanya vizuri katika maeneo mbalimbali.

Maadili hayo ni kumjali mteja, uaminifu, kufanya kazi kwa pamoja, weledi na uwazi," alifafanua Kashimba ambaye hivi karibuni alipokea tuzo ya mshindi wa kwanza katika kundi la watendaji wakuu bora kutoka taasisi za umma.

Kashimba aliwahakikishia wanachama wa PSSSF kuwa mfuko unafanya kazi kwa weledi wa hali juu hali inayosababisha kupokea tuzo mbalimbali ikiwamo hiyo ya uandaaji bora wa mahesabu.

Naye Lupi akizungumzia tuzo hiyo, alisema: "Kwa kweli namshukuru Mungu, watumishi wote wa PSSSF hususani wa Kurugenzi ya Fedha kwa kuwezesha kupatikana kwa tuzo hii.

Tuzo hii iwe chachu ya kuhakikisha kwamba mahesabu yetu yanaandaliwa vyema kila wakati".

Utoaji wa tuzo hizo ulishuhudiwa na Asmaa Resmouki, Rais wa Shirikisho la Kimataifa la Wahasibu (IFA), waalikwa kutoka nchi jirani na watendaji wa taasisi mbalimbali.

NBAA ilikuwa na kikao chake cha mwaka jijini Dar es Salaam kuanzia Novemba 29 hadi Desemba Mosi, mwaka huu, uliohudhuriwa na wahasibu na wakaguzi na kuhitimishwa na sherehe ya utoaji wa tuzo za umahiri katika uandaaji wa taarifa za fedha.

## HABARI KITAIFA

# Polisi yakiri chanzo ucheleweshaji haki

**Na Idda Mushi,** IRINGA

KAMISHNA wa Polisi, Kamisheni ya Uchunguzi wa Kisayansi, Shaban Hiki, amesema licha ya Ofisi ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali kufanyia kazi kwa wakati sampuli inazozipokea, wataalamu na askari wa upelelezi huchelewa hadi mwaka kuzichukua na kuchelewesha haki kutendeka.

Amesema licha ya kuwapigia simu na kuwaandikia barua ili wafuate majibu, wakati mwingine majibu hayo hukaa miezi sita hadi mwaka bila kuchukuliwa na kwamba tatizo hilo pia ni chanzo cha mrundikano wa majadala ya mashauri ya haki jinai ambayo hayafanyiwi kazi.

Kiongozi huyo alitoa kauli hiyo mjini Iringa jana akizungumza na wadau wa mnyororo wa haki jinai, wakiwamo askari polisi, mahakimu, madaktari na waendesha mashtaka wa mkoa wakati wa mafunzo maalum yaliyolenga kuhakikisha usalama wa uchukuaji, usafirishaji na utunzaji wa sampuli za uchunguzi wa kimaabara.

Kamishna Hiki alisema changamoto hizo zimeilazimu Mamlaka ya Mkemia Mkuu wa Serikali Kanda ya Kati Dodoma, kujadiliana na wadau hao.

Alisema lengo ni kupata uelewa wa pamoja na kusaidia haki kutendeka mahakamani kwa kuwa na ushahidi wa kisayansi kwa wakati badala ya ulie wa maneno wa kukiri.

"Ili haki itendeke kule mahakamani, siku hizi wanahitaji ushahidi wa kisayansi. Ule ushahidi wa zamani wa kukiri bila kuunganishwa na ushahidi wa kisayansi haupo tena.

Vielelezo vinavyochukuliwa eneo la tukio mara nyingi vikienda kuchakatwa kule maabara na kufanyiwa ulinganisho, humuunganisha mtuhumiwa na kosa alilofanya," alisema.

Kamishna Hiki alisema Jeshi la Polisi na Ofisi ya Mkemia Mkuu wa Serikali waliweka maazimio na kukubaliana kila mmoja kuwa na ofisa maalum ambaye kila siku asubuhi atawasiliana kujua ni sampuli ngapi zimetoka mikoani bila kupitia maabara ya polisi kwenda kwa mkemia mkuu.

Alisema lengo pia ni kujua taarifa ngapi zilizokamilika kutoka kwa mkemia mkuu ili ziende kwa mtumiaji ambaye ni ofisi ya RCO (Mkuu wa Upelelezi Mkoa).

"Wakishapata majibu huwa wanatuletea zinapita hapa lakini uzoefu unaonyesha ofisi ya mkemia mkuu hukamilisha kazi mapema na kwa wakati. Tatizo limebaki kwetu polisi.

"Majibu kutoka kwa mkemia mkuu yanakaa muda mrefu. Tuna ushuhuda majibu yanakaa miezi sita hadi mwaka mzima. Licha ya kuwapigia simu na kuwaandikia barua ili wafuate majibu, bado wamekuwa wanachelewa," alisema.

Kamishna Hiki alitoa wito kwa wakuu wa upelelezi wa mikoa na wilaya pamoja makamanda wa polisi mikoa kuzungumza na wapelelezi ili pindi wanapopeleka vielelezo ofisi ya mkemia au maabara ya polisi wajue kazi yao haijakamilika.

Aliwataka waendelee kuwasumbua kuhakikisha taarifa zinapatikana kwa wakati na kuondoa milolongo ya majalada ambayo hayajakamilishwa ili kwenda kwa mwanasheria wa serikali au mahakamani ili haki itendeke.

Meneja wa Maabara ya Mamlaka ya Mkemia Mkuu wa Serikali, Kanda ya Kati, Gerald Mollel, alisema lengo la mkemia mkuu ni kutoa mafunzo kwa kundi hilo ni kuhakikisha sampuli zinachukuliwa, zinatunzwa na kusafirishwa kwa usahihi ili kutoa majibu chanya yatakaosaidia kutoa hukumu ya haki kwa mashauri mbalimbali mahakamani.

Mollel alisema mafunzo hayo yamekuja wakati muafaka ambapo baadhi ya majibu ya sampuli yamekuwa yakichelewa kuchukuliwa, kuchukuliwa sampuli isiyotosheleza na kiwango kuwa chini cha utoaji wa majibu.

Vilevile, alisema kutowekwa nyaraka sawa, lebo au kupelekwa kwa sampuli zilizoharibika na kutotoa majibu yanayotakiwa, hivyo kufanya haki isitendeke vizuri na wakati mwingine kuwaachia watuhumiwa.

Alisema mamlaka hiyo yenye ithibati ina mitambo mizuri iliyowekezwa kwa gharama kubwa na serikali na kuwezesha upimaji wa hali ya juu wa sampuli kimataifa, hivyo hata mtu akitenda kosa, majibu ya kisayansi huwa ni sahihi.

Kuhusu majibu, alisema wamekuwa wakifanya kazi kwa kuzingatia miongozo ya huduma kwa mteja na hufanya kazi kwa sehemu yao, hivyo ni muhimu kwa Jeshi la Polisi kuyafuata kwa haraka ili kuwezesha haki kutendeka.

Naye Mkuu wa Mashtaka Mkoa wa Iringa, Basilius Namkambe, alikiri ucheleweshaji majibu ya vipimo kwa sampuli zinazohitajika kama ushahidi mahakamani kuwa kumekuwa kukishusha hadhi ya ushahidi husika na kufanya maswali mengi kuhusu kilichosababisha majibu hayo kushindwa kupelekwa kwa wakati.


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA YA TANZANIA

Katika mahakama ya mwanzo ya wilaya MOROGORO

Kituo cha KIHONDA Mkoa wa MOROGORO

Shauri la Madai/Ndoa Na. 128/2023

Jina la Mdai: HUSSEIN AL SAID SHOIRA

Jina la Mdaiwa: ASHURA OMARI MZERU

KUITWA SHAURINI MDAIWA
(Kanuni ya 18 ya kanuni za taratibu za madai katika Mahakama za mwanzo)

Kwa: ASHURA OMARI MZERU
0714-095555

Kwa kuwa Mdai/Wadai ameleta/Wameleta madai yake/yao kwamba: **MADAI YA FEDHA YA REDIO SABUFA YENYE THAMANI YA TSHS 330,000/=**
Kwahiyo unatakiwa kuhudhiria binafsi katika mahakama hii tarehe 5 Mwezi 12 Mwaka 2023 Saa 2:30 Asubuhi/mchana kwa mujibu wa madai hayo vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.
**ANGALIZO:** kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini, Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila ya wewe kuwepo.
Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 30 Mwezi 11 mwaka 2023.



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**MRADI WA UENDELEZAJI WA BONDE LA MSIMBAZI**
**(IDA CREDIT NO. 7215-TA)**

**TANGAZO KWA UMMA**

**KUSAINI MIKATABA YA MALIPO YA FEDHA ZA KUSAIDIA KUPATA ARDHI MBADALA KWA WATU WANAOATHIRIKA NA MRADI WA UENDELEZAJI WA BONDE LA MSIMBAZI**

Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI) inatekeleza mradi wa uendelezaji wa Bonde la Msimbazi kwa lengo la kukabiliana na mafuriko na kuboresha matumizi ya ardhi katika eneo la chini la bonde. Ili kufanikisha utekelezaji wa mradi, Serikali inatarajia kuwahamisha watu wote wanaoathirika na mradi kwa kuwalipa fidia ya mali zao zinazoathirika.

Serikali, kupitia tamko la Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – TAMISEMI la tarehe 15/11/2023, imeamua kuwalipa waathirika wote wanaohamishwa malipo sawa kwa ajili ya kuwasaidia kupata ardhi mbadala. Kampuni ya kusimamia ulipaji wa fidia (PROPERTY MATRIX LIMITED), inayofanya kazi kwa niaba ya OR-TAMISEMI, inatarajia kufanya zoezi la kusainisha mikataba ya malipo sawa kwa ajili ya kupata ardhi mbadala kwa waathirika wote ambao wameafiki malipo yao katika zoezi la mwezi Oktoba 2023. Kampuni hii itafanya zoezi hili katika kila Kata na Mtaa kwa ratiba ifuatayo:

| KATA | MITAA INAYOHUSIKA | TAREHE |
|---|---|---|
| Mchikichini | Msimbazi Bondeni | 6 hadi 7/12/2023 |
| | Misheni Kota<br>Ilala Kota | 8 hadi 9/12/2023 |
| Kariakoo | Kariakoo Kasikazini | |
| Upanga Magharibi | Charambe | 10 hadi 11/12/2023 |
| Jangwani | Mtambani A<br>Mtambani B | |
| Magomeni | Suna | 12 hadi 14/12/2023 |
| Mzimuni | Idrisa<br>Mtambani<br>Mwinyi Mkuu | |
| Kigogo | Kigogo Mbuyuni | 15 hadi 16/12/2023 |
| Hananasifu | Mkunguni A<br>Mkunguni B<br>Hananasifu | |

Wahusika wanaombwa kufika katika maeneo ya usainishwaji wakiwa na vitambulisho (NIDA/Uchaguzi) na nyaraka zote zinazowathibitisha iwapo wanapokea malipo kwa niaba.

**KATIBU MKUU**
**OFISI YA RAIS - TAMISEMI**

# Atamani wabunge walipwe 700,000/-

**Na Thobias Mwanakatwe,**
MKALAMA

MWENYEKITI wa Halmashauri ya Wilaya ya Mkalama mkoani Singida, James Mkwega, amesema kama angefanikiwa kuingia Ikulu, kitu ambacho angekifanya ni kufyeka mishahara ya viongozi wakubwa, wakiwamo wabunge kwa kuwalipa Sh. 700,000 kwa mwezi.

Aidha, amesema kundi ambalo angelilipa mshahara mkubwa ni wenyeviti na watendaji wa vitongoji, vijiji na kata.

Mkwega alitoa kauli hiyo juzi wakati wa maadhimisho ya kutimiza miaka 10 tangu kuanzishwa Halmashauri ya Wilaya ya Makalama Julai, 2013 baada ya kumegwa kutoka Wilaya ya Iramba.

"Siku moja nilikuwa na bosi mmoja wa Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISENI) (anataja jina). Sijui siku hizi ameshastaafu? Akaniambia hivi wewe mwenyekiti unalalamika serikali za mitaa, mfano wewe ungepewa urais ungefanya nini?

"Nikamwambia nikisaini tu Ikulu kazi yangu ya kwanza ni kuweka mishahara kwa wenyeviti na watendaji wa vitongoji, vijiji na kata na madiwani. Halafu baada ya kufanya hivyo ninafuta mishahara mikubwa ya Ma-DAS (Katibu Tawala wa Wilaya), wakurugenzi wa halmashauri wawe wanalipwa mshahara mdogo, wabunge ndio kabisa ninafikiri watabakiwa wakilipwa Sh.700,000," alisema.

Mkwega alisema angelipa mishahara mikubwa wenyeviti na watendaji kwa kuwa, kazi zikifanywa kwa ufanisi huko chini, viongozi wa juu hawatakuwa na kazi za kufanya.

Alisema wakati mwingine kumekuwa na mzigo katika utekelezaji wa majukumu kwa sababu kazi hazifanyiki kwa ufanisi ngazi za chini, lakini ikiwa mwenyekiti wa kitongoji analipwa Sh. 200,000 au 300,000 kwa mwezi angefanya kazi yake vizuri ili asipoteze mshahara huo.

"Lakini bahati mbaya kupewa Ikulu haiwezekani hata kuota tu kwamba kuna siku nitafika Ikulu hata kukaribishwa tu kama wenzetu walivyokaribishwa wakala na kunywa, mimi sijui kama nitakuja kukaribishwa ndio tatizo hilo," alisema.

Mkwega alisema anayasema hayo kutokana na kutambua kazi kubwa zinazofanywa na viongozi wa serikali za mitaa na kuwataka waendelee kutekeleza majukumu yao kwa kushindana kwani kutatolewa zawadi kwa viongozi wa vitongoji, kijiji na kata watakaokuwa wamefanya vizuri kazi zao.

Aliwataka wenyeviti hao kuitisha vikao vya serikali za halmashauri ya kijiji na mkutano mkuu kwa kuwa, vipo kisheria ili kumfanya Mkurugenzi wa Halmashauri afikirie vinginevyo dhidi yao.

Kaimu Ofisa Mipango wa Halmashauri ya Wilaya ya Mkalama, Daniel Tesha, alisema mafanikio yaliyopatikana katika halmashauri kipindi cha miaka 10 ni kuongezeka ukusanyaji mapato kutoka Sh. milioni 247.4 mwaka 2013/2014 na kufikia Sh. bilioni 1.749 mwaka 2022/2023, ikiwa ni ongezeko la asilimia 70.7.

Alisema katika kipindi hicho halmashauri hiyo ilifanikiwa kupata hati safi tisa na moja yenye mashaka na kwamba, mafanikio hayo yametokana na usimamizi mzuri wa kitengo cha fedha, uhasibu, menejimenti na Baraza la Madiwani.



Waokoaji wakipakia gari dogo aina ya Toyota Lactis yenye namba za usajili T 940 EZH lililopata ajali baada ya kugongana na lori namba T 320 DLH aina ya Iveco yenye tela namba T 514 AGW, katika barabara kuu ya Tanga - Segera eneo la Taasisi ya Utafiti wa Mifugo, jijini Tanga usiku jana na kusababisha kifo cha dereva wa gari dogo. **PICHA: HAMIDA KAMCHALLA**

VITA UKEKETAJI

# Mangariba wabadili mbinu kukwepa mkono wa sheria

**Na Waandishi Wetu**

WAKATI vita dhidi ya mangariba wanaowafanyia mabinti ukeketaji na kuhatarisha maisha yao vikiendelea, katika hali isiyo ya kawaida, kundi hilo limeibuka na mbinu mpya ya kutumia tumbaku.

Kwa muda mrefu sasa kumekuwa na kampeni ya kuelimisha mangariba ili kuachana na vitendo vya ukatili dhidi ya mabinti ambao wamekuwa wakiwakeketa na baadhi yao kupoteza maisha kutokana na kupoteza damu nyingi.

Wakati kampeni hizi zikiendelea hasa katika maeneo ambayo yalionekana kushamiri kwa vitendo hivyo, baadhi ya mangariba wamebainika kufanya ukeketaji kwa siri na wengine kuvuka mipaka ya nchi ili kukwepa mkono wa sheria.

Daktari Bingwa wa Watoto, Julieth Kabengula, kutoka Hospitali ya Rufani ya Kanda ya Kati ya Benjamin Mkapa (BMH), katika mahojiano na mwandishi wa habari hizi, anafunguka mangariba walivyobadili mbinu na sasa wanatumia tumbaku katika kutekeleza azma yao hiyo.

"Ni hatari kubwa kwa mangariba wanaowafanyia ukeketaji watoto wadogo kwa kupekecha sehemu za siri kwa kutumia tumbaku kwa sababu huwasababishia watoto kupata maambukizi mbalimbali ikiwamo homa. alisema kila kiungo cha mwanamke kina kazi yake huku akihoji kwa nini mangariba wanawafanyia mabinti ukeketaji.

"Ninaomba jamii iache tabia ya kukeketa watoto kwa kutumia tumbaku. Ni hatari kwa sababu husababisha mtoto kupata maambukizi ya magonjwa mbalimbali," alisema.

Mtaalamu huyo wa afya aliwataka wazazi na walezi kuacha kuwapeleka watoto kwa magharibа kwa kuwa kila kiungo cha mwanadamu kina kazi yake katika mwili.

Alisema binti anapokeketwa, miongoni mwa athari atakazopata ni pamoja shida wakati wa kujifungua, kusikia maumivu wakati wa tendo la ndoa na mengine ambayo humtokea baada ya kuwa mkubwa.

**DAWATI LA JINSIA**

Katibu wa Dawati la Jinsia kutoka Jeshi la Magereza, Scholastica Ndunguru, alisema wamekuwa wakipigia kelele ukeketaji kwa watoto na mangariba wamekuwa wakiipekecha tumbaku katika sehemu za siri za mtoto baada ya kuipasha kwenye moto.

Alisema wamekuwa wakitoa elimu kwa mangariba wote kuhusu madhara ya ukeketaji kwa njia hiyo katika baadhi ya mikoa kama Manyara na Mara ambayo imekithiri kwa vitendo hivyo.

Kwa mujibu wa Ndunguru, baada ya kuwabana kufanya vitendo hivyo, hivi sasa mangariba wengi wanavuka nje ya mipaka ya Tanzania na watoto kwenda kuwakeketa na baadaye kuwarudisha nchini.

"Sisi madawati ya jinsia tunapiga vita mila hizi potofu. Tunafanya jitihada mbalimbali zikiwamo za kuzungumza na wazee na mangariba wenyewe ili kuachana na dhana hiyo potofu," alisema.

Nduguru alisema watu wanaofanya vitendo hivyo wanapaswa kuacha mara moja kwa sababu wanawasababishia watoto madhara mbalimbali mwilini ikiwamo kupata maambukizi ya magonjwa huku akisisitiza vitendo hivyo ni vya ukatili na wahusika wanapaswa kuchukuliwa hatua kali.

**MA-RPC WAFUNGUKA**

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mara, Salum Morcase, akizungumza na Nipashe jana kwa njia ya simu alisema hajawahi kukutana na kesi ya mangariba kutumia tumbaku.

"Hatujawahi kukamata mtu ambaye amefanyiwa nje ya mipaka ya nchi na kurudishwa baada ya kufanyiwa. Hatuwezi kuthibitisha mpaka tumpate mtu athibitishe kuwa amefanyiwa mfano Kenya na kurudi Tanzania, kauli hizo mtaani zipo, tunazifanyia kazi," alisema.

Hata hivyo, Kamanda Morcase alisema kwa kipindi cha miezi sita hawajapata kesi mpya zaidi zilikuwapo ambazo zinaendelea mahakamani na zingine mangariba wameshatiwa hatiani na wanatumikia kifungo.

"Nilikwenda gerezani kutoa elimu madhara ya ukeketaji na ukatili nimekutana na mangariba ambao wamefungwa wako kama watatu. Kwa mkoa wetu mbinu za ukeketaji hutumika za kijadi za kutumia kisu na matendo hayo walikuwa wanafanya alfajiri sana wakiwa na vibuyu na vitu vingine mangariba hutumia kama desturi yao ya kimila ilivyo. Wapo waliokuwa wanatumia vijembe vilivyonolewa sana," alisema.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Manyara, Kamishna Msaidizi (ACP) George Katabazi, alisema kwa wastani kwa mwezi wamekuwa wakiwakamata mangariba wawili tofauti na awali idadi ilikuwa hadi wanne.

"Huwa tunawakamata mangariba lakini hiyo njia ya kutumia tumbaku hatujawahi kuwakamata. Yawezekana wakawa wanaitumia lakini sijawahi kupata kesi ya aina hii pengine mikoa inayolima tumbaku. Huku kwetu njia inayotumika ni ya kutumia wembe na vifaa vingine," alisema.

Alisema katika kampeni za kupinga ukatili ukiwamo ukeketaji huwa wanakwenda na mangariba waliokiri kuacha na huwa wanatoa ushuhuda na kukemea.

Oktoba 9, mwaka 2023, katika mkutano wa kimataifa wa kutokomeza ukeketaji, Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima, alisema matukio ya ukeketaji yanahitaji kukabiliwa kwa uzito mkubwa.

Dk. Gwajima alisema mataifa duniani yanahitaji kuwa na nguvu ya pamoja ya kulinda wanawake milioni 68 duniani walio katika hatari ya kukeketwa, milioni 50 wakitokea nchi za Afrika.

Alikiri kwa kiwango kikubwa kuwapo kwa tatizo la ukeketaji kwa mtindo wa kuvusha watoto na wanawake mipakani na kwenda kuwakeketa.

Kwa mujibu wa Mkakati wa Taifa wa Kutokomeza Ukeketaji 2020/21-2024/25, unaonesha Tanzania imejiwekea lengo la kupunguza kiwango cha ukeketaji kutoka asilimia 10 ya mwaka 2015/16 hadi kufikia asilimia tano ya mwaka 2024/25.

Taarifa ya Utafiti wa Afya ya Uzazi na Mtoto na Viashiria vya Malaria Tanzania 2015/16, inaonesha matukio hayo yameenea katika mikoa ya Manyara (asilimia 58), Dodoma (asilimia 47), Arusha (asilimia 41), Mara (asilimia 32), Singida (asilimia 31) na Tanga (asilimia 14).



Mkurugenzi Mkuu wa Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF), Dk. John Mduma (katikati), akizungumza kwenye kikao kazi baina ya mfuko huo na majaji, watendaji wa Mahakama na watendaji kutoka Tume ya Usuluhishi na Uamuzi (CMA), jijini Arusha jana. Kulia ni Jaji Mfawidhi wa Mahakama Kuu Divisheni ya Kazi, Dk. Yose Mlyambina na Jaji Mfawidhi wa Mahakama Kuu Kanda ya Arusha, Joachim Tiganga. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mahakama ya Kazi, WCF kushirikiana mabadiliko sheria fidia wafanyakazi

**Na Mwandishi Wetu,**
ARUSHA

MAHAKAMA Kuu ya Tanzania Divisheni ya Kazi, imesema iko tayari kushirikiana na Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF) kufanyia marekebisho baadhi ya sheria zinazohusu masuala ya fidia, ili kuboresha utoaji huduma kwa walengwa.

Jaji Mfawidhi wa Mahakama hiyo, Dk. Yose Mlyambina, aliyasema hayo jana jijini hapa wakati wa kikao kazi baina ya WCF na majaji, watendaji wa mahakama kutoka Kanda ya Kaskazini na Watendaji wa Tume ya Usuluhishi na Uamuzi (CMA).

"Naamini tutaendelea kuiboresha kwa kina sheria yetu kwa manufaa yetu sisi kama Watanzania. Sisi waheshimiwa majaji, waheshimiwa naibu wasajili na wasuluhishi wote, tuko tayari kutoa mawazo yetu kutokana na uzoefu tunaoupata kazini kwa ajili ya kuboresha sheria yetu ya Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi," alisema.

Jaji Mlyambina alisema anatamani WCF iwe mfano wa kuigwa si tu barani Afrika bali duniani kote katika masuala ya fidia kwa wafanyakazi na alishukuru Bodi ya Wadhamini ya WCF kwa kuisimamia vyema taasisi hiyo.

"Hakika wanatekeleza vyema majukumu yao kwa faida ya Watanzania. Mtakubaliana na mimi elimu tuliyoipata hapa kwa siku zilizopita ina mchango mkubwa sana katika kuiboresha Sheria ya Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi. Hii si tu kuwa ina manufaa kwa mfuko bali kwa Watanzania wote," alisema.

Naye Jaji Mfawidhi wa Mahakama Kuu ya Tanzania, Kanda ya Tanga, Katarina Mteule, alisema mfuko una faida kubwa kwa wafanyakazi, sheria zinaendelea kuboreshwa na hivyo ana mataumaini makubwa kuwa wafanyakazi watanufaika zaidi na mfuko.

Mkurugenzi wa Tume ya Usuluhishi na Uamuzi (CMA), Usekelege Mpulla, alisema kikao kazi hicho kina manufaa makubwa kwa kuwa wote kazi yao ni kuwahudumia waajiri na waajiriwa.

"Yako baadhi ya mashauri yanakuja kwenye tume lakini kuna wale ambao wanaleta mashauri ya kuumia kazini wanaweza kuhudumiwa na mfuko. Kubadilishana taarifa kunawawezesha wananchi kuhudumiwa kwa wakati," alisema.

Mkurugenzi Mkuu wa WCF, Dk. John Mduma, aliwashukuru majaji na washiriki wote kwa ushiriki wao.

"Bila shaka katika siku mbili za mafunzo mmepata picha halisi ya namna mfuko ulivyo na unavyofanya kazi zake, lakini kwa upande wetu tumepata nafasi nzuri ya kujifunza mengi kutoka kwenu na tunawaahidi ushirikiano na kufanya kazi kwa karibu na Mahakama Kuu ya Tanzania Divisheni ya Kazi.

"Mimi kwa niaba ya manejimenti na Bodi ya Wadhamini, tunaahidi kuyachukua mapendekezo mliyoyatoa ili kuboresha sheria yetu." Alibainisha.

Alisema mfuko umeanza kuyafanyia kazi mapendekezo ya waheshimiwa majaji kuhusu sheria mbalimbali zinazohusu fidia kwa wafanyakazi.

# ATCL kuanza safari moja kwa moja London

**Na Joseph Mwendapole**

SHIRIKA la Ndege Tanzania (ATCL), limetangaza kuwa liko kwenye maandalizi ya mwisho ya kuanza safari za moja kwa moja kwenda London, Uingereza kwa kutumia ndege yake ya Boeing 787-8 Dreamliner, mapema mwakani.

Pia imesema linatarajia kuendelea kuongeza miruko ya kwenda Mumbai, India na Guangzhou, China na kuanzisha safari mpya za Dubai, Muscat, Lagos nchini Nigeria, Kinshasa na Goma Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DRC).

Mkurugenzi Mtendaji wa ATCL Mhandisi Ladislaus Matindi, aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati wa uzinduzi wa Air Tanzania APP ambayo ni huduma inayopatikana kwenye simu za aina zote yaani zile zinazotumia mifumo ya "android" na zile za "ios".

Alisema Air Tanzania App inamleta msafiri kwenye ulimwengu halisi wa wasafiri wa anga na kumpa uzoefu wa pekee wa faragha na uhuru wa kuchagua.

"Air Tanzania App si tu kwa ajili ya kuwezesha safari bali pia, inamuwezesha mteja wa Air Tanzania kunufaika na ofa za bidhaa mbalimbali pamoja na kupata huduma za nyongeza," alisema.

"Kupitia Air Tanzania App, mteja ataweza kuchagua muda wa safari, daraja la safari, kiti, kununua begi la ziada mahali popote ulipo, muda wowote unapohitaji kusafiri kwenda sehemu yoyote ndani na nje ya nchi ambapo Air Tanzania inafanya safari zake," alisema.

Matindi alisema mteja anayetumia Air Tanzania App ataweza kulipia na kupata tiketi yake ya safari papohapo ambapo kwa sasa ataweza kupatiwa huduma kwenye vituo 15 vya ndani ya nchi na 11 nje ya nchi.

"Tunakusudia kuongeza vituo vya Pemba, Tanga, Mafia, Nachingwea, na Musoma na kurudisha safari za Iringa na Mtwara kwa mtandao wa safari za ndani ya nchi ili kuwawezesha wadau wengi kunufuaika na uwepo wa Air Tanzania," alisema.

Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania (TAA0, Musa Mbura, alisema ili kupata matokeo tarajiwa ya bidhaa mpya sokoni ni muhimu kufanya upembuzi yakinifu kabla ya kuiingiza bidhaa hiyo sokoni.

"Matokeo ya taarifa ya upembuzi yanawezesha kupata picha halisi inayosaidia kufanya uamuzi sahihi, hivyo ni imani yangu, uamuzi wa kuanzisha Air Tanzania App ulipitia mojawapo ya hatua hii," alisema.

Aidha, alisema hatua hiyo inaendana na kuwekeza mtaji sahihi katika bidhaa ili kuongeza uwezo wa ushindani katika soko na kuleta matokeo yenye tija.

"Bidhaa mliyoitambulisha leo, imekuwa ikisubiriwa kwa hamu na sisi wateja wenu hata mimi binafsi na niwapongeze sana kwa namna mlivyoandaa hafla hii, haya ni maandalizi ya kiwango cha hali ya juu na inaonesha utayari wenu katika kuitambulisha Air Tanzania App," alisema.

Alisema APP hiyo inaonyesha namna Air Tanzania ilivyojipanga kushindana kwa viwango vya kimataifa kwani lengo la matumizi ya teknolojia ni kurahisisha upatikanaji wa huduma.

Alisema Air Tanzania App itarahisisha upatikanaji wa tiketi za safari na kumpa mteja faida za nyongeza na itawaleta wasafiri kwenye ulimwengu halisi wa teknolojia na kuwapa hadhi ya pekee na kuwapongeza kwa kupiga hatua hiyo ya kutumia kwa usahihi mapinduzi ya teknolojia.

"Ninaamini kuwa Air Tanzania App imefanyiwa majaribio ya kutosha na kujiridhisha kuwa mtaweza kukabiliana na idadi kubwa ya wateja wenu pale watakapotumia App hii. Naamini haitalemewa na changamoto za kuzidiwa kimtandao (network traffic)," alisema.

## Aliyehitimu udaktari na umri mdogo atoboa siri

**Na Joseph Mwendapole**

MHITIMU wa fani ya udaktari ambaye ni mdogo kuwahi kutokea tangu kuanzishwa kwa Chuo Kikuu cha Kumbukumbu ya Hubert Kairuki (HKMU), Ahlam Azam Mohamed, ametoa siri ya namna alivyofanikiwa kuhitimu akiwa na miaka 21.

Akizungumza na Nipashe jana baada ya mahafali ya 21 ya chuo hicho, Mikocheni, Dar es Salaam, Mohamed alisema alimaliza darasa la saba akiwa na umri wa miaka 13 na baada ya hapo hakuendelea na masomo ya darasani, kwa maana ya sekondari.

Alisema baba yake alikuwa akimletea walimu wa masomo mbalimbali nyumbani ambao walimfundisha kwa miezi minne na kumudu kufanya mtihani wa kidato cha nne katika Shule ya Sekondari ya Al Muntazir kama mtahiniwa binafsi.

"Nilisomea nyumbani masomo ya sekondari ya kidato cha kwanza hadi cha nne kwa miezi minne kisha nikasoma masomo ya kidato cha tano na sita ndani ya mwaka mmoja, kwa hiyo nilimaliza masomo ya kidato cha sita nikiwa na miaka 15.

"Nilijaribu kujiunga na vyuo lakini majibu yalichelewa kwa hiyo nikalazimika kusubiri mwaka mzima, nikaja kujiunga na masomo ya udaktari hapa Kairuki mwaka 2018 nikiwa na miaka 16. Nafurahi leo (jana) hii nimehitimu udaktari," alisema.

Mihanmed alisema alivutiwa kusomea nyumbani baada ya kumwona kaka yake amefanikiwa kusoma masomo hayo ya kidato kwanza hadi cha nne akiwa nyumbani na kufaulu kwenye mitihani yake.

Awali, Makamu Mkuu wa HKMU, Prof. Yohana Mashalla, alisema chuo kinaona fahari kwa mara ya kwanza kuwa na mhitimu mdogo wa fani ya udaktari kuwahi kutokea tangu kuanzishwa kwa chuo hicho.

Prof. Mashalla alisema mhitimu huyo alijiunga na chuo hicho mwaka 2018 na amekuwa akifanya vizuri zaidi kwenye masomo yake yote na kupata shahada ya udaktari.

"Tulijaribu kupekua pekua kwenye maeneo mbalimbali nchini kuangalia kama kwenye vyuo vya wenzetu hapa nchini kuliwahi kuwa na mhitimu wa fani ya udaktari mwenye umri kama huu lakini ilionekana kwamba mbali na HKMU, hapa nchini huyu ni wa kwanza," alisema.

Kwenye mahafali hayo, wahitimu walikuwa 308 na mmoja alitunukiwa Shahada ya Uzamivu ya Sayansi, yaani Doctor of Science (Honoris Cause), 13 Stashahada ya Ustawi wa Jamii, 82 Stashahada ya Uuguzi, 14 Shahada ya Ustawi wa Jamii, 35 Shahada ya Uuguzi na 150 Shahada ya Udaktari wa Binadamu.

Wahitimu wawili walitunukiwa Shahada ya Uzamili ya udaktari wa binadamu katika tiba ya afya ya watoto, watatu Shahada ya Uzamili ya Upasuaji, watatu Shahada ya Uzamili ya Magonjwa ya Wanawake na uzazi na sita Shahada ya Uzamili ya Tiba.

MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Matokeo kuhusu Ukimwi yasitufanye tushangilie

**SERIKALI** juzi ilizindua matokeo ya awali ya Utafiti wa Viashiria vya Matokeo ya Ukimwi Tanzania kwa mwaka 2022/23 ambayo yanaonyesha kiwango cha ushamiri wa maambukizi mapya ya virusi vya Ukimwi (VVU) kwa watu wenye umri wa miaka 15 yanaendelea kupungua.

Matokeo hayo yaliyozinduliwa mkoani Morogoro na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, wakati wa maadhimisho ya Siku ya Ukimwi Duniani yaliyoadhimishwa kitaifa mkoani Morogoro, yanaonyesha miongoni mwa watu wazima wenye umri wa miaka 15, maambukizi hayo yanaendelea kupungua kutoka watu 72,000 waliokuwapo mwaka 2016/17 hadi watu 60,000 kwa mwaka 2022/23.

Sambamba na kupungua kwa maambukizi hayo kwa vijana ambao ni nguvu kazi ya taifa, ripoti hiyo inaonyesha kuwa wastani wa maambukizi ya Virusi vya Ukimwi kwa Tanzania Bara ni asilimia 4.5 na kwa Zanzibar 0.4 na kwa upande wa jinsia, wanawake kiwango cha maambukizi ni asilimia 5.6 kulinganisha na wanaume asilimia 3.0. Pamoja na kuonesha kuwa kiwango kwa wanawake kiko juu, sababu imebainika kwamba hawajitokezi kupima ili kujua hali ya afya zao.

Habari njema zaidi zinaonyesha kuwa kwa mujibu wa utafiti, kiwango cha kufubaza VVU kinaendelea kukua kwa wastani wa asilimia 78. Kwa wanawake kiwango kimekua kwa asilimia 80.9 na wanaume asilimia 72.2 ikilinganishwa na asilimia 52 iliyokuwapo kulingana na utafiti wa mwaka 2016/17.

Pamoja na matumaini hayo ya kupungua kwa maambukizi, mikoa ya Iringa, Njombe na Mbeya bado inaongoza nchini katika kiwango cha maambukizi ya VVU huku Njombe ikiwa ya kwanza kwa asilimia 12.7. Mkoa ambao maambukizi yako chini kuliko yote ni Kigoma kwa asilimia 1.7.

Kutokana na utafiti huo, ni kweli jitihada katika mapambano dhidi ya Ukimwi na maambukizi mapya ya VVU zineonyesha kutia matumaini. Licha ya matumaini hayo, jitihada zaidi zinatakiwa kwa sababu kama kutakuwa na dalili yoyote ya kujisahau, mambo yanaweza kubadilika na kuwa kama zamani.

Kwa vijana kwa mfano ambao bado wako katika hatari ya kukumbwa na janga hilo, jitihada zaidi zinahitajika ikiwamo kutoa elimu kuhusu kinga. Kupungua maambukizi kwa kundi hilo, kusiwe furaha kama msemo usemao mgema akisifiwa tembo hulitia maji. Kama alivyosema Waziri Mkuu, ni wakati mwafaka kwa vijana nchini kuanza kujitambua na kutathmini maisha yao kwa kujikinga na maambukizi mapya ya VVU.


Mbali na kuwasihi vijana kuendelea kujikinga, pia ni muhimu kwa wale waliopimwa afya na kubainika kuwa na VVU, waendelee kutumia dawa za kufubaza virusi (ARV) ili kuendelea kuwa na afya njema pamoja na kujikinga na magonjwa nyemelezi ambayo huchochea kuongeza vifo vya watu wa kundi hilo.

Kwa mikoa ya Iringa, Njombe na Mbeya ambayo imeeleza kuwa bado inaongoza kwa viwango vya maambukizi, inapaswa kutupiwa jicho la kipekee ili kuongeza kazi ya mapambano na kupunguza viwango hivyo. Ni imani kwamba mikoa hiyo imeonekana kwa upekee wake, hivyo kama jitihada za makusudi zitaelekezwa, ni hakika mambo yatakuwa tofauti katika utafiti ujao.

Kwa ujumla. Ukimwi bado ni janga ambalo limeangamiza kwa kiasi kikubwa nguvu kazi ya taifa, hivyo ni vyema Watanzania kwa ujumla wakachukua tahadhari na kuzingatia maelekezo yanayotolewa kuhusu ugonjwa huo. Kama alivyosema Rais wa Awamu ya Nne, Dk. Jakaya Kikwete, kuwa Tanzania bila Ukimwi inawezekana, kauli hiyo inaweza kutimia kama kila mmoja atasimama katika nafasi yake kwenye mapambano dhidi ya ugonjwa huo.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Mwaka 2024 huo, udhibiti utoro kidato cha kwanza uanze mapema

Na Sabato Kasika

**MWAKA** 2023 unaelekea ukingoni na Januari mwaka ujao, panapo majaliwa, wanafunzi wa kidato cha kwanza watakuwa wanaanza masomo yao ya sekondari katika shule mbalimbali za serikali na binafsi nchini.

Kabla mwaka huo haujaanza, ninadhani kuna haja ya kukumbusha tatizo ambalo huwa linajitokeza kila mwaka wakati wa kuanza kidato cha kwanza ambalo ni wanafunzi kutohudhuria masomo.

Limekuwa kama jambo la kawaida baadhi ya wanafunzi wanaochaguliwa kuanza kidato cha kwanza kutoripoti katika shule walizopangiwa, huku kukiwa hakuna taarifa zozote za kutoripoti.

Mtindo huo umekuwa ukisababisha serikali za wilaya na mikoa katika maeneo yenye utoro kuchukua hatua mbalimbali zikiwamo za kuanzisha msako dhidi yao, ili wapatikane waende shuleni kuendelea na masomo.

Inawezekana wako wale ambao wazazi wao huwahamishia katika shule zingine badala ya zile walizochaguliwa, lakini ninadhani si wengi, kwani inawezekana shule moja wanafunzi zaidi ya 200 hawajaripoti.

Kwa hesabu hiyo, sidhani kama idadi hiyo yote wanaweza kuwa wamehamishiwa shule nyingine, bali inawezekana kuna utoro ambao unatakiwa kutafutiwa chanzo chake mapema na kupatiwa ufumbuzi.

Wakati mwingine inawezekana miongoni mwa wanaofaulu ni wale wasio na mwamko wa elimu au ugumu wa maisha, wazazi kuwaozesha binti zao au kuruhusu wakafanye kazi za ndani wapate cha kulisha familia.

Vilevile, inawezekana wengine wanalazimishwa na wazazi wasio na mwamko wa elimu, kubaki wakifanya shughuli za nyumbani, hivyo wanadhani elimu ya msingi inatosha.

Aidha, mazingira ya sekondari za kata yanaweza kuwa chanzo cha utoro, kwa kutokuwa na mazingira rafiki kwa wanafunzi, kwa kukosa mabweni, umbali mrefu na pia ubovu wa miundombinu ya shule zenyewe.

Kimsingi hilo halina ubishi, kwani unakuta mwanafunzi anatembea umbali wa kilomita tisa hadi 10 kwenda shule, halafu shuleni hakuna hakuna walimu wa kutosha, wala vifaa vya kujifunzia na kufundishia.

Lakini pamoja na hayo yote, sidhani kwamba yanaweza kuwa kigezo cha mwanafunzi kuacha kwenda shule, kwani wapo waliosoma katika mazingira hayo na wakafanya vizuri.

Hivyo, ingekuwa vyema kama wazazi na walezi watawakazania watoto wao kwenda shule wakati taratibu nyingine za kuboresha mazingira ya shule zikiendelea, badala ya kuruhusu wawe watoro.

Ni vyema pia kukumbusha kuwa shule za serikali ni za umma, hivyo umma hauna budi kuzihudumia ili zilwe katika mazingira mazuri kwa manufaa ya watoto wao badala ya kujiweka pembeni.

Ninadhani umefika wakati wa kutafuta mapema ufumbuzi wa kudumu wa utoro huo unaojitokeza kila mwaka, kwani sidhani kama ni sahihi wanafunzi kuziona sekondari za kata kana kwamba haziwafai.

Shule hizo zimekuwa ni mkombozi wa watoto wa maskini na ninaamini wapo waliofika mbali kupitia shule hizo. Hivyo, wazazi na wanafunzi wanaochaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza na kufanya utoro, wangeachana na mtindo huo usio na manufaa maishani.

Pamoja na changamoto katika shule hizo, elimu bado ni ya muhimu, hivyo, kwa kuwa serikali inaendelea kuboresha miundombinu ya shule hizo, ni muhimu wanafunzi kutokubali kuwa watoro.

Hivyo, ushirikiano unahitajika kutoka kila upande, serikali iboreshe mazingira ya shule ili yawe rafiki kwa wanafunzi, wazazi nao watambue umuhimu wa elimu na kutoruhusu watoto wao kuwa watoro.

Mwezi wa mwisho kwa mwaka 2023 ndio huu, hivyo, ungetumika kuangalia mazingira yote yanayochangia kuwapo kwa utoro na kuyatafutia ili mwaka ujao kusiwe na msako wa wanafunzi watoro.

SAFU

FIKRA MBADALA

# Tuondoe kwanza ubatili huu ndani ya katiba yetu



Pascal Mayalla

LEO naendelea na uchambuzi wangu wa muswada huu wa Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani wa mwaka 2023, kwa mukhtasari wa sura zote 10, kuwaelimisha elimu ya uraia na elimu ya sheria na haki. Lengo ni kuwawezesha Watanzania kuwa na ufahamu kuhusu sheria hii.

Pia kwa kuifahamu huko, itakuwa fursa murua kwa Watanzania kutumia kikamilifu miezi miwili iliyobaki ya kutoa maoni na mapendekezo ya maboresho ya sheria hii. Wiki iliyopita nilichambua sura ya nne mpaka ya sita na leo naendelea na sura ya saba mpaka ya 10

Sura ya Saba ya Muswada inaweka masharti kuhusu makosa mbalimbali yanayoweza kutendwa wakati wa uandikishaji, uteuzi wa wagombea na uchaguzi. Miongoni mwa makosa hayo ni pamoja na kutumia wadhifa kushawishi watu wengine kutoomba kuteuliwa, mwenendo usiofaa wa watendaji wa uchaguzi na maofisa waandikishaji, makosa yanayohusu fomu za uteuzi au karatasi za kura, vitendo vya ushawishi na rushwa.

Makosa mengine ni kutotunza siri katika uchaguzi kwa watu wanao ruhusiwa kuwa katika kituo cha kupigia kura au kuhesabia kura na kuingilia mikutano halali ya hadhara. Sambamba na kuainisha makosa mbalimbali, sehemu hii inaweka pia adhabu kwa mtu atakayetenda makosa hayo.

Ili jambo hilo liende vizuri, maini yangu Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) iendeshe elimu kwa umma kuhusu makosa ya uchaguzi na taratibu za kufuatwa kutuma malalamiko. Huwa kunatokea malalamiko mengi kuhusu uchaguzi kwa kuripotiwa kwenye vyombo vya habari, lakini ukija kufuatilia NEC, unakuta hakuna malalamiko yoyote yaliyoripotiwa. Sura ya Nane ya Muswada inaweka masharti kuhusu kupinga matokeo ya uchaguzi kwa njia ya shauri la uchaguzi. Kwa mujibu wa sura hii, mashauri ya uchaguzi kupinga matokeo ya ubunge yatasikilizwa katika Mahakama Kuu na mashauri ya uchaguzi kupinga matokeo ya udiwani yatasikilizwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi. Miongoni mwa taratibu zilizoainishwa katika sura hii ambazo mtu aliyefungua shauri atapaswa kuzingatia ni utaratibu wa kuweka dhamana ya gharama. Aidha, sehemu hii inaweka pia masharti ya mamlaka ya Jaji Mkuu kutengeneza kanuni zitakazosimamia usikilizwaji wa mashauri ya kupinga matokeo ya uchaguzi. Ili kuhakikisha ufanisi katika utekelezaji wa kanuni hizo, inapendekezwa kuwa kanuni hizo zitengenezwe kwa kushauriana na NEC. Maoni yangu, kuhusu dhamana ya gharama, Tanzania lazima tufike mahali haki ifanywe kuwa stahili na stahiki. Kiwango cha dhamana kisiwe kikwazo cha upatikanaji wa haki kwa wasio na uwezo.

Maadam serikali imeanzisha taratibu za msaada wa kisheria kwa wasio na uwezo, utaratibu huu pia ufanyike kwenye kesi za uchaguzi. Kwa vile kwenye katiba pendekezwa tulikubali hadi matokeo ya urais kupingwa mahakamani, kwa nini tusianze sasa kwenye sheria hii?

Sura ya Tisa ya Muswada inahusu masharti ya jumla ambayo yanajumuisha mamlaka ya Mkurugenzi wa Uchaguzi na Wasimamizi wa Uchaguzi kupata taarifa, malipo ya watendaji wa uchaguzi, mamlaka ya NEC kutengeneza kanuni kwa ajili ya utekelezaji bora wa sheria na matumizi ya teknolojia katika utekelezaji wa majukumu mbalimbali ya tume.

Sura ya 10 ya Muswada inaweka masharti kuhusu kufutwa kwa Sheria ya Taifa ya Uchaguzi ya mwaka 1985 na Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa ya Mwaka 1979 na kuweka utaratibu kwa masharti yatakayoendelea kutumika hata baada ya kufutwa kwa sheria hizo.

Sheria hizo zina vipengele batili vinavyokwenda kinyume cha Katiba ya Tanzania ya mwaka 1977. Vipengele hivyo ni pamoja na mgombea kudhaminiwa na chama cha siasa. Uanachama wa chama cha siasa ni hiari lakini haki ya Mtanzania kuchagua na kuchaguliwa ni haki ya msingi. Kwa nini kumlazimisha Mtanzania akitaka kugombea ni lazima ajiunge na chama cha siasa?

Mchungaji Christopher Mtikila (Mungu amweke mahala pema peponi) mwaka 1993, alifungua kesi Na. 5 ya 1993 kupinga kifungu hiki na Mahakama Kuu kupitia kwa Jaji Kahwa Lugakingira (Mungu amweke mahala pema peponi) ikatamka wazi na bayana kipengele hicho ni batili na kinakiuka katiba ya JMT ya mwaka 1977, hivyo kifutwe na kutoa haki kwa kila Mtanzania kuwa ana haki ya kushiriki kugombea uongozi.\ Serikali ilikata rufani, ikashindwa. Hapa ndipo serikali yetu ikafanya sarakasi kupeleka bungeni kwa hati ya dharura Sheria No. 34 ya mwaka 1994, kufanya marekebisho ya 8 ya Katiba kukichomeka kipengele hicho ndani ya Katiba.

Mahakama Kuu chini ya majaji watatu, (majaji watatu kisheria inaitwa Half Bench), Amiri Manento, Salum Masati na Thomas Mihayo, wakayakubali mambo yote ya Mchungaji Mtikila na kumpa ushindi tena kwa kutamka marekebisho hayo ya katiba ni batili!

Lakini serikali ikakata tena rufani na safari Mahakama Kuu hii ikakaa jopo la majaji saba (Full Bench) Jaji Mkuu mwenyewe, Agustino Ramadhani, akisaidiwa na majaji Eusebia Munuo, January Msoffe, Natalia Kimaro, Mbarouk Salum Mbarouk, Bernard Luanda na Sauda Mjasir. Juni 17, 2010 ikatoa hukumu ya ajabu kabisa kuwa kutokea Tanzania! Katika kutoa uamuzi huo, mahakama haikuwa peke yake, bali iliwaita mabingwa wabobezi wa sheria na katiba kuisaidia. Hawa ni wanaitwa marafiki wa mahakama, kwa kiingereza ni 'friends of the court', kisheria Amicus Curiae, ambao ni Othman Masoud Othman, Prof. Palamagamba Kabudi na Prof. Jwan Mwaikusa (Mungu aiweke roho yake mahala pema peponi).

Uamuzi wa Mahakama ya Rufani uliamua kitu cha ajabu sana na hapa naomba ninanukuu

"So as to let the will of the people prevail as to whether or not such (independent) candidates are suitable. We are definite that the Courts are not the custodian of the will of the people. That is the property of elected Members of Parliament".

Hii kiukweli ni kauli ya ajabu sana kutolewa na mahakama yetu kwenye jambo zito na muhimu kama hili. Kitendo cha Mahakama kujivua jukumu la kuwa the custodian of the will of the people, ni kitendo cha ajabu sana na kushangaza sana. Hakuna will of the people kubwa kuliko katiba!, kama katiba imetoa haki fulani, halafu Bunge likatunga sheria ya ajabu kabisa kuifuta haki hiyo, halafu mahakama ikatamka haiwezi kuliingilia Bunge!, where is the doctrine of separation of powers, checks and balance?.

MADONGO YA MGAGAGIGIKOKO

# Ushindi kwa mbeleko ni kuendekeza aibu



Na Joseph Kulangwa (kulangwasos@gmail.com)

WAPENZI wa michezo hususan wa masumbwi, Jumamosi iliyopita ya Novemba 25, bila shaka saa za jioni hadi usiku, walikuwa ama ukumbini au mbele ya televisheni zao wakishuhudia masumbwi yaliyokuwa yakipigwa katika ukumbi wa hoteli ya Mount Meru, Arusha.

Pambano kuu la usiku huo liliwahusu Mtanzania Abdallah Pazi 'Dulla Mbabe' na Mkongomani, Eric Katompa, lililokuwa la raundi 10 lililomalizika huku Katompa akipewa ushindi wa alama za majaji watatu waliokuwa wakilisimamia.

Ni dhahiri matokeo hayo yalisikitisha Watanzania nikiwamo mimi kwani ingawa ilikuwa mara ya pili Dulla anapoteza kwa Katompa, lakini kutokana na utanzania na uzalendo, bila shaka hakuna aliyekuwa tayari kushuhudia matokeo hayo.

Lakini kwa walioilitazama vizuri pambano hilo, ni wazi 'Dulla Mbabe' hakuonesha ubabe wake mbele ya Mkongomani karibu katika kila raundi, ingawa yeye alisema alifanya vizuri raundi ya kwanza hadi ya tatu. Ukweli ni kwamba alichakazwa na kujikuta akimkumbatia kila mara mshindani wake huyo aliyeonekana kuwa makini.

Tushukuru, kwamba kuna vyombo vya habari hususan televisheni, ambavyo vimekuwa vikituonesha mapambano mbalimbali situ ya masumbwi, bali hata michezo ambayo awali haikuwa ikioneshwa, lakini sasa inaoneshwa yakiwamo masumbwi.

Hata hivyo, baada ya kumalizika kwa mapambano hayo hususan baada ya Dulla kupoteza kwa Katompa, mmoja wa wanamasumbwi nguli nchini, Ibrahim Class alionekana akilia sana kuliko hata aliyepoteza, akionesha kuguswa na mchezo huo, hasa kushindwa kwa Dulla.

Hiyo si siri kwani siku hiyo kila yalipokuwa mapumziko ya wanamasumbwi hao, Class alitoka kwenye meza ya wachambuzi na kwenda kwenye kona ya Dulla kumpa mawaidha ya nini afanye ili kushinda mchezo ule.

Hakika pamoja na urafiki wake na Dulla, Class alionesha utanzania akitaka kuulinda dhidi ya ukongo, ambao ulikuwa umebebwa na Katompa. Hata alipohojiwa na mtangazaji, Class alijikuta akilaumu majaji kwa kutombeba Dulla.

Alitolea mfano wa nchini Ujerumani akisema huko Mjerumani akiwa ulingoni akipambana na mgeni, hata alipopigwa na 'kulamba sakafu', alitangazwa mshindi kulinda hadhi ya nchi, Class akilalamika kuwa 'uzalendo' huo haupo Tanzania, akitaka Dulla angalau angebebwa hata na majaji hata kama alionesha dhahiri kushindwa!

Yawezekana alishikwa na jazba baada ya kuona kipenzi chake kikipoteza, ingawa hakika haikuwa kauli mwafaka kwa mchezaji nyota kama yeye aliyejizolea umaarufu duniani, kutaka mtu abebwe hata kama ameshindwa, kwa sababu tu anachezea kwenye ardhi ya Tanzania na majaji ni Watanzania. Si sawa!

Hata hivyo, Class alijirudi siku moja baadaye na kuomba radhi kwa kauli ile, nampongeza kwa uungwana huo aliouonesha, hasa nikitambua kuwa ni uchungu tu ndio ulimkuta na kujikuta akitoa kauli ile, ingawa kauli ya mtu maarufu hubebwa nzima nzima.

Yawezekana pia ni katika ule utaratibu wa kuomba radhi lakini ujumbe umefika, jambo ambalo kwa kweli linaweka alama mbaya katika tasnia ya michezo, ambapo kwa kauli ile, wasimamizi wa michezo hususan ya masumbwi nchini wangeshughulika naye kinidhamu.

Ieleweke, kuwa michezo ni siasa, michezo ni urafiki, michezo ni udugu lakini michezo pia ni diplomasia kwa sababu hiyo kauli kama ya Class ingekumbatiwa, ingeweza kutuvuruga na wenzetu wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC) anakotoka Katompa.

Aliyoyasema Class yalipata kujitokeza huko nyuma, ambako endapo Mtanzania alicheza na mgeni lakini isitokee KO, basi Mtanzania hata kama alipigwa kisawasawa na kuzidiwa alama alipewa ushindi na hata kuondoa ladha ya mchezo huo ambao hivi sasa una mashabiki lukuki nchini.

Wachezaji wetu wawe wa masumbwi au hata soka na michezo mingine, wajue kuwa kinachoangaliwa uwanjani au ulingoni, ni ujuzi wa kukabiliana na mshindani wako na si kusubiri kubebwa ili kupata ushindi, jambo hilo kama litafanywa na majaji au waamuzi, basi tujiandae kufa kimichezo.

Ni vizuri viongozi na wachezaji tunapokabiliwa na michuano ya michezo, ni bora tukajiandaa kimwili na kiakili kukabiliana na washindani na kuwashinda, badala ya kusubiri kubebwa kwa sababu tu tuko uwanja au ulingo wa nyumbani.

Tukiendekeza tabia hii, itakuja kutokea siku tukataka kubebwa hata kwenye riadha na wasimamizi kwa sababu kwa mchjezo wenyewe haitawezekana, siri kuu ni uwezo na mbinu za ushindi zisizohusisha kubebwa au imani za kishirikina. Sitaki kuamini kwamba Class na Dulla Mbabe walikuwa wakisubiri mbeleko kwa Katompa.

Tuwaulize wanamasumbwi wa zamani kama kina Habib Kinyogoli, Willy na Makoye Isangura, Rashid Matumla na wengine, walikuwa wakisubiri kubebwa ili wapate ushindi ulingoni badala ya kutumia nguvu na akili.

Dulla jipange tu upya siku hazifanani na mbeleko si suluhisho.

**Kazi Iendelee.**

# Taasisi yapigia debe vijana, wanawake uongozi

**Na Elizabeth Zaya**

SHIRIKA la Utunzaji wa Mazingira, Haki za Binadamu na Jinsia (ENVIROCARE), limesema kuna haja ya kuwaamini vijana na wanawake katika nafasi za uongozi. Katika mafunzo ya wanafunzi kutoka vyuo mbalimbali pamoja na wanasiasa, Meneja Mradi wa Uongozi kutoka shirika hilo, Godlisten Muro, alisema bado makundi hayo hayajapewa nafasi vya kutosha katika nafasi za uongozi.

Alisema katika uchaguzi ujao kuanzia wa serikali za mitaa mwakani na uchaguzi mkuu mwaka 2025, ni vema makundi hayo yakajitokeza kwa wingi kugombea nafasi za uongozi na kuwaomba wapigakura kuwaamini kwa kuwapigia kura ili wakaonyeshe uwezo wao.

"Tunajua vijana na wanawake wana uwezo mkubwa wa kuongoza isipokuwa bado hawajapewa nafasi. Tumeona hata wale wachache wanaopewa nafasi hizo wanafanya vizuri, kwa hiyo wakiwa wengi wataleta mageuzi makubwa katika demokrasia ya Tanzania," alisema Muro.

Alisema kikwazo kingine kinachokwamisha wasijitokeze kwenye kuwania nafasi mbalimbali hususani za kisiasa ni ukosefu wa kipato.

"Ziko baadhi ya nafasi hasa za kisiasa ambazo ili ugombee ni lazima uwe na kipato, hiyo ni changamoto kubwa sana iliyopo. Kwa hiyo hilo nalo linawakwamisha sana hasa vijana," alisema Muro.

Meneja kutoka Shirika la Forum CIV, Kusini na Kaskazini mwa Afrika, Jackson Obare, alisema Tanzania inafanya vizuri katika eneo la demokrasia licha ya kuwapo na maeneo machache ya kufanyia kazi.

"Tunafahamu kwamba kila nchi huwa ina mfumo wake wa kidemokrasia na kwa Tanzania bado inafanya vizuri katika eneo hilo japokuwa ni maeneo machache sana ya kuboresha, tunaamini kadri miaka inavyokwenda mambo yataendelea kuwa mazuri zaidi," alisema Obare.

Mshiriki wa mafunzo hayo kutoka kundi la wenye ulemavu, Mariam George, alisema bado kumekuwa na hali ya kutoshirikishwa kwa kundi hilo katika mambo mbalimbali ikiwamo kwenye mikutano na vikao vya uamuzi kuanzia kwenye serikali za mitaa.

Alisema wao wana haki ya kushirikishwa katika kila jambo na kwamba wataendelea kudai haki hiyo.



Wahitimu wa Chuo Kikuu cha Hubert Kairuki (HKMU), wakiandamana wakati wa mahafali ya 21 ya chuo hicho, Dar es Salaam jana. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Mganga Mkuu Dar awapa neno wanafunzi CBE

**Na Joseph Mwendapole**

MGANGA Mkuu wa Jiji la Dar es Salaam, Dk. Zaituni Hamza, amewataka wanafunzi wa Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE) kuwa makini na masuala ya uhusiano wa kimapenzi na badala yake waangalie zaidi masomo.

Aliyasema hayo jana wakati wa maadhimisho ya Siku ya Ukimwi Duniani yaliyofanyika chuoni hapo.

Aliwataka wanafunzi wa chuo hicho kujihadhari na ugonjwa wa Ukimwi kwani kwa kufanya hivyo wanakuwa wameepuka maradhi mengine ambayo yanaweza kukatisha uhai wao.

"Kwa wasichana mnapoepuka ngono zembe unaepuka mambo mengine kama mimba ambazo hazikutarajiwa kwasababu unaweza ukajikuta unaahirisha masomo au kushindwa kuendelea unapopata hali hiyo," alisema.

Alisema mtu anapotaka kuanzisha uhusiano anapaswa kutulia na kujiuliza aina ya mtu anayetaka kuwa naye badala ya kukurupuka na kuchukua mtu ambaye hawatadumu naye.

"Wahenga walisema majuto ni mjukuu. Kwa hiyo usikurupuke kuingia kwenye uhusiano kwa sababu lazima ujue changamoto zako na ujue ni mtu gani anaweza kuzivumilia na mfahamiane vya kutosha ili kusiwe na majuto ya kusema ningejua nisingeingia kwenye uhusiano huu," alisema.

Aliongeza kuwa uhusiano mwingi wa kimapenzi umekuwa na changamoto nyingi ambapo vijana wengi wameathirika kisaikolojia baada ya kugundua kuwa wameingia sehemu ambazo hazikuwa sahihi kwao.

"Tumeshuhudia vijana wengi wakichukua uamuzi wa kujiua sababu ya uhusiano wa kimapenzi.

Kwa hiyo acheni kushirikisha moyo badala ya kufikiri kwa kina kama uhusiano huo utakufaa au la," alisema.

Mganga Mkuu huyo pia aliwataka wanafunzi hao washiriki kwenye programu atamizi na ya uanagenzi ili wawe mahiri kwenye masomo na kupata ajira kwa urahisi wanapomaliza chuo.

Alisema waajiri wengi wanazingatia umahiri wa mwajiriwa kwenye utendaji wa kazi hivyo aliwaasa kuzingatia elimu kwa vitendo kwa kuwa ndiyo itawapa ujuzi wa kutosha kuweza kujiajiri na kuajirika kirahisi wanapomaliza masomo.

"Waajiri wengi kwa sasa huwa hawaangalii vyeti wanaangalia uwezo wako wa kufanya kazi kwa hiyo mnapomaliza chuo na kuja huku mtaani mjipange kweli kweli hakikisheni mna ujuzi wa kutosha.

"Waajiri wengi wanataka watu wabunifu na wepesi wa kutambua na kutatua changamoto zinazotokea kwenye taasisi zao kwa hiyo hakikisheni mnakuwa wabunifu na wepesi wa kufanyakazi kwa bidii ili kutatua changamoto zinapotokea," alisema.

Mshauri Msaidizi wa Wanafunzi wa CBE, Marco Stephano, alisema wamekuwa wakiadhimisha siku hiyo kila mwaka kuwakumbusha wanafunzi kuhusu hatari ya ugonjwa wa Ukimwi na maradhi mengine yatokanayo na ngono zembe.

Alisema siku hiyo wamekuwa wakifanya shughuli mbalimbali ikiwamo kutoa ushauri nasaha kwa wanafunzi wa chuo hicho kuhusu namna ya kujikinga na ugonjwa huo hatari wa Ukimwi.

"CBE ina wanafunzi wengi sana kwa hiyo chuo imeona ni busara kuwa kinaadhimisha siku hii kwa kufanya shughuli mbalimbali kama kutoa ushauri nasaha kwa wanafunzi kuhusu umuhimu wa kuachana na ngono zembe na kujikinga na mimba zisizo tarajiwa ili wajikite zaidi kwenye masomo yao," alisema.

# UDSM yajitosa kukuza ubunifu

**Na Mary Geofrey**

CHUO Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) kimetoa mafunzo maalumu kwa wanafunzi wabunifu ili kuwajengea mtazamo chanya kuhusu ubunifu na ujasiriamali.

Mkurugenzi wa Ubunifu na Ujasiriamali wa UDSM, Prof. Hannibal Bwire, akizungumza na waandishi wa habari juzi kuhusu mafunzo ya ubunifu na ujasiriamali kwa wanafunzi, alisema kuwa na sera nzuri ni jambo la msingi na muhimu.

Prof. Bwire alisema kwa kutambua changamoto zilizoko katika sekta hiyo chuo hicho kimeona ni muhimu kuanzisha mafunzo hayo ili kukuza bunifu nchini.

Alisema mafunzo hayo ni ya kuwakuza wanafunzi na wabunifu wengine katika kile wanachokifanya kwa kufuata taratibu.

"Changamoto ziko nyinyi, mfano rasimali watu na fedha kwa sababu kuna mbunifu anaweza kuwa amefikia mahali ambapo anatakiwa kuinuliwa ili kubiasharisha bidhaa au wazo lake lakini unakuta hakuna fedha," alisema.

Aidha, alisema zinahitajika sera zinazokidhi uhitaji katika sekta ya ubunifu, kupata masoko na kuifanya sekta hiyo kuwa yenye tija.

Mwakilishi Mwandamizi wa Shirika la Ushirikiano wa Kimataifa la Japan (JICA) linayoshirikiana na chuo hicho katika kutoa mafunzo hayo, Hitoshi Ara, alisema watatoa mafunzo hayo kwa siku tano kuhusu ubunifu na ujasiriamali.

"Tunatarajia kuwa na vikundi sita vya kushiriki katika programu hii ya muda mfupi na mashindano yatafanyika na vikundi hivi siku ya mwisho ya programu," alisema Ara.

Alisema baada ya mashindano hayo vikundi vitatu bora vitakuchukuliwa na kuwa chini ya mshauri wa JICA kwa miezi miwili na kundi moja bora litachaguliwa ili kupata uzoefu katika ubunifu na ujasiriamali kutoka Japan.

Mratibu wa ujasiriamali katika Kurugenzi ya Ubunifu na Ujasiriamali chuoni hapo, Dk. Winnie Nguni, alisema wanafunzi wengi wana uelewa na ujuzi katika ufundi wa bidhaa na kutengeneza mawazo, lakini wanakosa uelewa na maarifa ya namna ya kuyafanya mawazo au bidhaa zao kuwa biashara.

Alisema tatizo la ubunifu kuwa biashara inasumbua wabunifu wengi si vyuoni tu bali hata walioko mitaani.

# MAISHA

DESEMBA 3, 2023

Nipashe

Baba, Mama na Mwana

Jumapili


Ukurasa 14



## Unga wa ubuyu ni tiba

## MAISHA NI NYUMBA

Ukurasa 15






## KATUNIKA


Ukurasa 16



# SHEER ZAIDI YA VAZI

Ukurasa 13


## MAJIBU YA WIKI ILIYOPITA




| | | | |
|---|---|---|---|
| 3 | 1 | 4 | 2 |
| 4 | 2 | 3 | 1 |
| 1 | 3 | 2 | 4 |
| 2 | 4 | 1 | 3 |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| K | ■ | S | H | I | B | A |
| I | ■ | ■ | ■ | L | ■ | N |
| K | ■ | J | A | A | ■ | G |
| W | A | O | ■ | L | I | A |
| E | ■ | G | O | A | ■ | L |
| T | ■ | O | ■ | ■ | ■ | I |
| E | M | O | R | O | ■ | A |


## FUMBO TOTO



Jaza maneno yafuatayo katika vyumba vilivyo wazi:


NOA, MEE, EDA, ZEE, OGENI, ENEZA, MANDE, UMEME, ENDELEA, TANESCO

## TOA TOFAUTI 5



## AMSHA AKILI

MSAIDIE MCHWA AONE NJIA WALIYOPITA WENZAKE WALIOTANGULIA



## WATOTO

# PAKA RANGI




## CHEKA

SHUHUDIA jinsi mgambo walipokwenda kumkamata jamaa mmoja

**Mgambo:** Hodi, hodi
**Jamaa:** Kimya
**Mgambo:** Hodi, hodi wenye nyumbaa
**Jamaa:** We nani kwani?
**Mgambo:** Sisi mgambo
**Jamaa:** Sawa, mnataka nini?
**Mgambo:** Kuongea na wewe
**Jamaa:** Kuongea na mimi?!
**Mgambo:** Ndio
**Jamaa:** Mko wangapi?
**Mgambo:** Watatu
**Jamaa:** Kama mko watatu si muongee wenyewe...!!!

**SWALI**
Paka ana manufaa gani kwa binadamu?

## MAISHA NDIVYO YALIVYO

Na Flora Wingia



# Mke akikuvuruga mezea, wajali zaidi watoto wako!

KARIBU msomaji tuendeleze vituko vya baadhi ya wanawake dhidi ya waume zao. Baba mmoja akaniandikia kisa chake kupitia mtandao kwamba ana ndoa yenye miaka 25 na kubahatika kuzaa watoto watano lakini mwiba mkali.

Baba huyu akabahatika kwenda ulaya akawapatia pia watoto shule huko. Mkewe hakutaka kwenda ng'ambo kumbe alikuwa na ajenda ya siri.

"Nilipodadisi nikagundua uhusiano na mtu mwingine. Niliumia sana kwani nilimpenda sana mke wangu. Nikarudi ulaya kutuliza akili. Nifanyeje?

Walioshirikishwa jambo hili wakashauri hivi kumtuliza jamaa yetu aliyesema akiwa Ulaya anajawa na amani kuliko pale nyumbani kwake na mkewe aliyempenda mwenyewe na sasa amekuwa mwiba mkali.

Mshauri wa kwanza anasema; "Kwa kweli mimi binafsi nampa pole sana huyu jamaa, ila kilichounganishwa na Mungu mwanadamu hawezi kukitenganisha.

"Vijana wengi wanapopata nafasi kidogo hukimbilia kuoa bila kufanya uchunguzi wanaoa mwanamke gani. Hii husababishwa na mapenzi motomoto ya mwanzo wa penzi.

"Nimeona vijana wengi wamalizapo vyuo hukimbilia kuoa mapema na matokeo yake wanajuta. Siyo wanawake wote waolewao, bali wateule tu hata kama ni wazuri.

"Wanawake ni wajanja sana waonapo jamaa amesoma au ana mwelekeo wa kupata pesa hata kwa wakati ujao, au wanajitahidi kujenga mazingira ya kuoana. Suala hili linatugharimu sana sisi vijana tusio na uzoefu wa mapenzi.

"Mitego iwekwayo na wanawake wajanja wa mapenzi ni kujitambulisha kwa kila mtu kuhusu mahusiano yenu siku za mwanzo wa penzi. Hukushauri mwende mkasali ili ujue anamtanguliza Mungu katika mtego wake, kisa nawe uwe na hofu ya Mungu katika maamuzi yako.

"Yafaa uwe makini sana na watu aliokua na mahusiano hapo awali ili ujue ameachana nao au la. Wakati mwingine atakushauri mpunguze starehe kwa kujifanya anaandaa zaidi future, atakuomba ruhusa kutoka kwenda popote hata kama yupo kwao na mengine mengi. Ila ukitaka kujua yote hayo ni uongo au ni kweli mpe muda mrefu wa kuchunguzana lazima atarudia tabia zake halisi.

"Ushauri wangu kwa jamaa huyu ni kuvumilia na kufikiria zaidi watoto watano alionao. Pia kwenda kupima DNA, ili kujua kama watoto ni wake au analea watoto wa mume mwenzake.

"Misalaba duniani ni mingi kwa hiyo ndugu yangu vumilia hilo ndio chaguo lako, somesha watoto wako kama wewe unavyosoma, watoto wakiwa wakubwa mama yao atajirudi tu. Pia jitahidi mwende mkapime VVU. Hii inaweza kuwa njia muhimu ya kumjenga hofu mkeo ili atulie.

"Kumbuka pia kumpeleka kwa wazazi wake kwa mashauriano akaulizwe anachotaka aamue mwenyewe. Mwisho mtangulize Mungu mbele ili mkeo abadilike wala usifikirie kumuacha." Naitwa Pastory Stephano Simu, Sengerema.

Ujumbe mwingine unasomeka;-

"Napenda nichangie mada ya huyo baba aliyeingia mkenge! Kwanza kabisa ajue maisha ndivyo yalivyo kwani, kila mtu ana matatizo yake na asijione ni yeye tu wapo wengi wa aina hiyo.

"Namshauri atulizane, kama aliweza kuvumilia mpaka sasa ni takribani miaka 25, yeye ni jasiri. Mengi ya huyo mke ameyafahamu na kwamba hataki kwenda huko ng'ambo, pengine sababu ya huyo mshikaji.

"Vile vile mume huyo anasema huko ng'ambo ana amani kubwa sana. Mimi namwambia ashikilie hapo hapoooooooo! Kuna usemi wa siku hizi usemao raha jipe mwenyewe.

"Akiendelea kuwaza ya mkewe hata uzee wake utamjia vibaya, aendelee na mambo yake huko aliko, kwani sikio la kufa halisikii dawa. Ila asisahau kutunza watoto wake ambao sasa nafikiri ni wakubwa." (Dorry, Dodoma)

Hayo ndio maoni ya msomaji wetu wa pili. Kama unayo ya nyongeza karibu. Jeuri kubwa ya bibie ni kule kuwa na uhusiano wa nje. Hizo ndizo sekeseke za maisha, kila mtu ana mapito yake!

Mke huyu hakika ni kiruka njia. Ameruka ukuta na kutafuta wachuchu wa nje. Ni hatari sana. Iliyopo ni bwana yule aridhie moyo wake, ahangaikie wanawe waweze kusonga mbele waweze kujitegemea. Awasomeshe vema ili iwe ufunguo halisi wa maisha yao.

Raha ya mke ndiyo kama imefikia tamati. Afanyeje sasa? Hana hata sababu ya kumfuatilia mke huyu anayeonekana ni jeuri. Huko ni kumpenda asiyependeka!

***Je, una maoni, ushauri? Ujumbe 0715268581.***

## WARAKA WA NDANI

Na Godfrey Mushi



# 'Single mother' sawa, ukorofi wa nini?

UMEAMUA kuwa 'single mother'. Umeamua kuishi mwenyewe, hutaki mwenza, basi ishi kwa kutulia.

Purukushani ya nini, ugomvi wa nini? Kwa nini usiishi uhalisia wa maisha yako? Yaani wewe kutwa kisirani na wapangaji wenzako, mara majirani.

Najua uliishi katika mazingira ya kufanyiwa ukatili na kisaikolojia ukajikuta umeathirika kisaikolojia.

Hakuna asiyejua kwamba uzazi wa mpango ni uamuzi wa hiari wa mtu binafsi mke/mume au mtu na mwenzi wake kuhusu lini waanze kupata watoto.

Wanataka wazae wangapi, wapishane kwa muda gani, lini waache kuzaa na njia gani ya uzazi wa mpango wangependa kutumia. Wote tunakubaliana katika hilo.

Hakuna ubishi kwamba, ni muhimu kwa anayetaka kutumia uzazi wa mpango kufanya tathmini ya kina juu ya usalama na ufanisi wa kila njia.

Kwa sababu, si kila njia ya uzazi wa mpango inamfaa kila mtu, kila mtu ana njia yake kulingana na mazingira.

Huwezi kuamka tu na kwenda hospitalini unasema unaenda kuchoma sindano, kuweka kitanzi, kipandikizi au vidonge. Sharti kwanza, ujue njia zote na faida yake na kisha upime kulingana na umri na mazingira yake njia ipi itakufaa.

Nimesukumwa kuandika kisa hiki cha 'single mother' baada ya kuona katika vyombo vya habari, baadhi ya wanawake wakipaza sauti zao kwamba wamejikuta wakiishia kuwa single mother kwa sababu ya kukimbia ukatili.

Wengi wao wanalalamikia kukithiri kwa vitendo vya ukatili wa kingono, hasa ubakaji na ulawiti dhidi ya watoto, lakini pia wanawake kunyimwa haki ya kurithi mali.

Achilia mbali vipigo na ukatili wa kiuchumi dhidi ya wanaume kutajwa kuwa miongoni mwa matukio ya ukatili yanayoendelea kuota mizizi katika kata hiyo; chanzo ni wazazi kutokutimiza wajibu wao wa kutunza familia, ulevi uliokithiri, kutokuwa na elimu ya masuala ya haki za binadamu na matukio ya ukatili kutokushughulikiwa ipasavyo na vyombo vya dola.

Kubwa zaidi, wanaume wameeleza masikitiko yao kuhusu baadhi yao kufanyiwa na wenza wao ukatili kama kuwanyima 'unyumba' kwa sababu hawana pesa ya kuwahudumia.

Kibaya zaidi ni namna wake zao wanavyotekeleza kile walichokiita ukatili wa kisaikolojia dhidi yao, kwa kuweka vipandikizi vya uzazi wa mpango ili kuwazuia wasizae nao.

Tazama kauli hizi zinavyoumiza wanaume: "Unazungumza nini! sasa hivi watoto wako huku (anaonyesha kwa kupiga kwa mkono bega lake), nani ana muda wa kuzaa? Wanawake wanasema hawana muda wa kuzaa, wana muda wa kutafuta pesa.

"Nazungumza ukweli na Mungu anasikia. Wanafungia watoto huku (begani), hata ufanyeje hakuna mimba. Nyie kinamama muangalie mpange muda wa kuzaa kuongeza taifa."

Baada ya kauli hiyo, mwanamke mmoja jasiri akasimama akajibu: "Hatutaki kuzaa kwa sababu tunalea peke yetu. Nina mume ninabeba mimba peke yangu miezi tisa, naenda leba najifungua pale. Wakuja kuniangalie pale hakuna, natoka hospitalini narudi nyumbani natakiwa nile uzazi miezi mitatu, wa kuniangalia kwenye ule uzazi hakuna.

"Mtoto anakua anatakiwa malazi, anatakiwa elimu, haki zote za mtoto anatakiwa na anayezifanye zote ni mimi mwanamke. Nimeshazaa mtoto wa kwanza nimekiona, nimezaa wa pili nimekiona, hivi kweli nitathubutu kuongeza wa tatu na wa nne? Kwa hiyo ziko sababu zinazotufanya wanawake na mabinti tunaokua tutumie uzazi wa mpango."

Kwamba sasa hivi eti wanawake wa Uchagani hawaelewi somo, wameziba masikio na kwao ni mwendo wa matumizi ya sindano, vidonge, kitanzi na kutoshiriki ngono na waume zao.

Amkeni ninyi maofisa ustawi wa jamii, maofisa maendeleo ya jamii, Wizara ya Afya na Wizara husika ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, kuchangia uboreshaji wa msaada wa kisaikolojia, haki ya kielimu na kumaliza matatizo ya afya ya afya ya akili yanayosababishwa na kukithiri kwa ukatili wa kijinsia.

*•Godfrey Mushi, ni Mwandishi Mwandamizi wa Gazeti la Nipashe, Kanda ya Kaskazini. Anapatikana kwa simu namba 0715 545 490 au barua pepe: ghandsome79@gmail.com*


# HARUSI







Tukio la harusi ni jambo muhimu kwa wanandoa hasa unapoandaliwa jukwaa likiwa tofauti. Pichani ni baadhi ya harusi zilizo-andaliwa kitamaduni na kuonekana za kipekee zaidi.



# MITINDO





## 'SHEER' ZAIDI YA VAZI

KATIKA kipindi hiki cha joto mavazi mepesi yanapendwa zaidi kwa ajili ya kupunguza kero ya hali mbaya ya hewa.

Ni wazi mavazi mepesi yenye uwezo wa kuufanya mwili upumue na kuuweka salama dhidi ya jasho yanapendekezwa kutumiwa.

Moja ya vazi linalopendekezwa ni mashati penyezo, au wenyewe waniita 'Sheer' ambayo yana uwezo wa kumfanya mtu kujisikia furaha katika kipindi chote.

Mashati haya ambayo yana uwezo wa kuona nguo uliovalia ndani yanapendeza zaidi kuvaliwa na wanawake kwa kuwa yanamuongezea mvuto zaidi.

Wataalamu wa mavazi wanasema Sheer ni moja ya bidhaa muhimu katika nyakati za joto kwa kuwa idadi kubwa ya watu wanapenda kuwa nayo ili kupunguza usumbufu.

Unapovaa nguo hizi ni lazima uwe na nguo nyingine ya ndani kama fulana fupi, shumizi au nguo maalum ya kuhifadhi kifua kwa sababu sifa yake kuu ni kuwa ya wazi.

Pamoja na vazi hili kupendwa zaidi na watu wa Ulaya na Marekani, lakini katika nchi za Kiafrika linapendeza hasa kutokana na hali ya hewa kuwa ya joto kwa kipindi kirefu.

Shati la 'Sheer' halichagui aina ya nguo inayokwenda nayo sambamba, unaweza kuvaa sketi, suruali au jeans na viatu vya aina zote.

URREMBO

Na Mary Geofrey

# CHEKO SI HABA

HAKIKA kila mtu anahitaji kuwa na kicheko kinachovutia, je, utajuaje kama una mwonekano mzuri pale unapocheka?

Basi kiungo muhimu kinachofanya watu wapende kicheko chako ni mng'aro mwanana wa meno yako, kuanzia usafi na mpangilio wake.

Ukiwa maridadi unatakiwa kuna na meno meupee na sio yenye rangi, hivyo itakufanya kila wakati ukitabasamu na kufurahia na wenzako.

Leo tutaelekezana jinsi ya kusafisha meno ili kupata kicheko kinachopendeza.

**UTUNZAJI WAKE**

Inategemea ni vipi unatunza afya yako ya meno, kama unapiga mswaki vizuri au unasafisha vizuri.

Kama meno yako si ya rangi ile inayotakiwa, chagua kati ya hizi njia mbili za kutumia mara moja kila wiki.

Njia hizo ni kusafisha meno kwa kutumia baking soda na juisi ya ndimu na mafuta ya nazi.

Baking soda ina Sodium Bicarbonate ambayo inasaidia kuondoa madoa na rangi, pia juisi ya ndimu inasaidia kupunguza alkaline iliyopo kwenye meno.

Changanya juisi ya ndimu pamoja na baking soda kupata mchanganyiko mzito

Futa meno kuondoa majimaji kisha chukua mswaki wako, chota mchanganyiko kisha paka kwenye meno. Usipige nayo mswaki kama unavyotumia dawa ya meno, wewe paka tu.

Iache kwa dakika moja kisha sukutua na maji safi, fanya hivyo mara moja kwa muda wa wiki.

**TUMIA MAFUTA YA NAZI**

Tumia mafuta ya nazi kila asubuhi kusukutua kabla hujapiga mswaki.

Weka kiasi cha kutosha mdomoni kisha anza kusukutua, zungusha katika kila kona, fanya kama unavuta na kuyasukuma mdomoni lakini usiyameze.

Fanya hivi kwa dakika 10 hadi 15. Ukishamaliza sukutua kisha piga mswaki kama kawaida.

Dawa hizi zina uwezo wa kulinda meno na wadudu na kuyatakatisha.





MAPISHI

Na Mary Geofrey

# Unga wa ubuyu ni tiba

UBUYU ni miongoni mwa tunda lenye faida nyingi ndani ya mwili wa binadamu.

Unga wa ubuyu unaelezwa kuwa na vitamini na madini mengi kuliko matunda mengine yoyote.

Katika mwili ubuyu una uwezo mkubwa wa kuimarisha kinga ya mwili, mifupa, kusaidia mfumo wa umeng'enyaji chakula, kupunguza maumivu na uvimbe na kusisimua utengenezaji wa seli na tishu mpya.

Pia husaidia kupunguza shinikizo la damu na kuzuia magonjwa sugu.

Inaelezwa kuwa unga wa ubuyu una vitamini C mara sita zaidi ukilinganisha na chungwa.

Ubuyu una kiwango maradufu cha madini ya Calcium kuliko maziwa ya ng'ombe. Pia madini mengine yapatikanayo katika ubuyu ni pamoja Chuma, Magnesium na Potassium ambayo ni mara sita zaidi ya ile Potassium ipatikanayo katika ndizi.

Huongeza au kuboresha nuru ya macho na kusaidia kuzuia kuharisha na kutapika.

Namna ya kutumia

Jipatie kikombe kimoja cha juisi ya ubuyu kila siku hasa usiku na baada ya wiki kadhaa utaona matokeo yake mwilini.

Ili upate faida za juisi ya ubuyu, jinsi inavyoelezwa, lazima upate ule ubuyu halisi usiochanganywa na kitu kingine cha kuongeza ladha au rangi.

Jinsi ya kuandaa juisi

Chukua unga wa ubuyu, weka kwenye kikombe, ongeza maji na ukoroge vizuri.

Unaweza kuongeza sukari au asali, tikisa na unywe ikiwa ya moto au baridi.





MAISHA NI NYUMBA

**Na Elizabeth Zaya**





# Unaiwekaje nyumba yako msimu wa sikukuu?

MSIMU wa sikukuu umewadia. Ni kipindi ambacho kinakuwa na pilikapilika za hapa na pale katika nyumba, kukiwa kunaonekana kutawala mapambo yanayoshabihiana na msimu wenyewe.

Katika ofisi na sehemu mbalimbali, ukipita au kuingia, unakutana na mapambo ya sikukuu ukiwamo mti wa Krismasi ukiwa ndiyo umetawala.

Katika makala hii ya nyumba, tunakupa dondoo kidogo kukuongezea baadhi ya vitu ambavyo vitachagiza msimu wako wa mwaka huu kuwa mzuri zaidi na ukaufurahia ukiwa nyumbani kwako.

Naamini kwamba katika kipindi hiki familia nyingi huwa zinaungana pamoja katika mapumziko ya mwisho wa mwaka, kwa hiyo ni muhimu kukifanya kipindi hiki kikawa ni cha furaha zaidi kwa mapambo tofauti ya sikuu ndani ya nyumba.

Mbali na mti wa Krismasi, lakini pia yako mapambo mengine tofauti hilo, kama hutoweza kupata mti, unaweza pia kutafuta aina nyingine ya mapambo ambayo huenda yasikugharimu kabisa au ukayapata kwa gharama kidogo.

Lengo ni kuhakikisha nyumba yako inachangamka na kuipa raha familia ambayo imekusanyika nyumbani kwa ajili ya mapumziko ya mwisho wa mwaka.

Unaweza kuchanganya na mapambo mengine tofauti kama 'wall papers' na maua mengine kwa kuzingatia rangi zinazoshabihiana na msimu wenyewe.

Kwa mfano mapambo mengine ambayo yanaweza kutumika Krismasi ni pamoja na karatasi za rangi, taa za kung'aa, mapambo ya karatasi yanayotengenezwa kwa mtindo wa nyota.

Mengine ni kengele za Krismasi, picha za kondoo, farasi, mipira ya kung`aa, wanyama wadogo wa kutengenezwa kama kondoo.

Mapambo mengine ambayo unaweza kutengeneza ni ya maua ya asili kwa kuyaweka katika chombo au chupa maalumu ambacho kinaweza kuwekwa hata juu ya meza.

Pamoja na kupendezesha nyumba, pia hewa na harufu hubadilika na kuwa nzuri zaidi kutokana na maua yanayowekwa ndani.

Unaweza kupamba pia maneno yenye ujumbe maalum ambayo unaweza kuyaandika mwenyewe ya kuendana na msimu au ukayanunua katika sehemu maalumu yanapopatikana.

Hakikisha unaweka mapambo sehemu ambayo ni salama na hayawezi kuharibika kwa namna yoyote au kuharibiwa na watoto.

Pia nyumba katika msimu huu inatakiwa iwe inapigwa nyimbo zinazoshabihiana na msimu wenyewe.

Baada ya kuisha kwa msimu unatakiwa uyaondoe na kudizaini upya mwonekano wa nyumba yako.

# Pangilia rangi za maua kuifurahia bustani yako

**Na Restuta James**

WATAALAMU wa bustani wanaeleza kuwa palipo na bustani pana rangi nzuri na utulivu. Hali hii inasababishwa na uwezo wa mtu kupangilia aina za maua alizonazo ili kutengeneza madhari na hisia ya kumtuliza mtu.

Wanaeleza kuwa namna mpangilio ndiye 'mchawi' wa kuifanya bustani ionekane nzuri na ya kuvutia ama vinginevyo.

Wanashauri kuwa mchanganyiko wa maua yanayochanua na yale yasiyotoa maua unaweza kuleta utulivu mkubwa na hivyo kusababisha furaha kwa mtu anayehitaji kupumzika kwenye eneo la nje.

"Rangi fulani husababisha hali fulani na kuongeza 'hisia' kwenye bustani. Mpangilio sahihi katika bustani yako hukuruhusu kuamua ni hali gani ungependa kuisikia kwenye mchanganyiko wenye kijani kibichi kwa wingi," anaeleza Peter Boniface, ambaye ni mtaalamu wa bustani.

Anashauri kuwa kwa watu wenye maeneo makubwa ya bustani, wanaweza kuyagawa kwa kupanda maua yanayoamsha hisia mahsusi kutokana na mpangilio wake.

Kwa wenye eneo dogo wanashauriwa kutumia maua ya kuning'iniza kutengeneza hisia stahiki.

**VIDOKEZO MUHIMU**


Kama hitaji lako ni kutengeneza hisia ya amani na utulivu, mtaalamu huyo anapendekeza kuwa kama una eneo kubwa la bustani, ni vyema mchanganyiko wa maua katika eneo hili uwe unaochanua maua ya bluu tulivu na maua meupe. Wataalamu wanaeleza kuwa mchanganyiko wa ukijani, bluu tulivu na nyeupe unasababisha hisia ya amani kwa mtu.

Kwa hisia za mapenzi au furaha, wataalamu wa bustani wanashauri mchanganyiko uwe na yale yanayochanua maua ya pinki na nyeupe. Ukumbuke kwamba maua haya yataratibiwa vyema na kijani kibichi kinachotawala bustani.

Kwa hisia za mvuto, wanashauri kuwa mchanganyiko wa maua mekundu, rangi ya machungwa na njano, ni muafaka kwa kuongeza hali hiyo.



# KATUNI


KATUNIKA KI'DOMOKRASIA
BY ABDUL KINGO - 2023
SMS - 0713 447766
JUKWAANI
LITAKUFA JITU 'NIPO PALEEEE! MIMACHO KODO!
NAIONA KABISA SAFARI YETU MBINGUNI INAVYOKUWA NGUMU, KUMBUKA WAMETUPIGIA KURA HAWA WATU!
KELELE UTAPALIWA! MAHUBIRI PELEKA KWENYE NYUMBA ZA IBADA SIO HAPA!
SISI
TUACHE DESTULI ZA ULIMBUKENI KILA MTU ACHEZE MECHI ZAKE
UTASABABISHA TUCHEKE WAKATI TULIKUWA HATUKO KWENYE 'MUDI HIYO' SEPA BHANA
TUTAMBUANE MWENZANGU UNAPOWAKAMATA WATU UNAWAPELEKAGA KITUO GANI?
ZAIDI YA KITUO CHA BASI SINAGA KWINGINE BABA!
NIMEKUPA LIFTI UMEFIKA LAKINI BADO HUTAKI KUSHUKA! SHUKA BHAMA
NIMEVUTA JIKO JIPYA KANISHUSHE MLANGONI NIPATE JINA UKWENI
HII NDIO SHIDA YA KUOA MKE TOKA 'KANDA MAALUMU! KILA KITU KIJESHIJESHI
SI KILANGA CHAKO! KWANI WAZARAMO WENZAKO HUKUWAONA? EMBU NAMBIE MIMI NA MPIRA NANI MKEO?
DONA'
MME WANGU MTU MWENYEWE NDO HUYU KILA MARA ANANTAKA' NIMECHOKA ANANTONGODHA SANA!
TUSHAURIANE UNGEPENDA NIZIKIWE HAPA HAPA AU WASAFIRISHE? KAMA HAKUNA JIBU TWENDE UKAJIFIKIRIE TUTARUDI
*KINYUNYIZO CHA LEO...
KILA MCHEZO HAUKOSI MATOKEO USINUNE...

## HABARI KIMATAIFA

# Israel yalipua maeneo 400 Gaza

**TEL AVIV,** ISRAEL

ISRAEL imeshambulia maeneo 400 ndani ya Ukanda wa Gaza, baada ya mapigano kuanza tena Ijumaa asubuhi.

Taarifa ya Jeshi la Israel (IDF), ilieleza vikosi vya angani, majini na ardhini vimelenga miji ya Gaza, ikiwamo ile ya maeneo ya kusini.

"Ndege za kivita zililenga zaidi ya shabaha 50 katika shambulio kubwa katika eneo la Khan Younis," ilisema taarifa hiyo.

Khan Younis ilikuwa shabaha nyingine ya vikosi vya Israel baada ya Gaza Kaskazini.

Taarifa hiyo ilisema kuwa mashambulizi ya anga yalilenga msikiti mmoja kaskazini mwa Gaza, kwa madai unatumiwa na kundi la Islamic Jihad kama kituo cha kuendesha vita.

Wakati huo huo, ripoti za vyombo vya habari zimefichua kuwa Waziri Mkuu wa Israel Benjamin Netanyahu anapanga kujenga uzio wa usalama ndani ya Ukanda wa Gaza baada ya vita kumalizika.

Kulingana na vyanzo viwili vya habari vilivyozungumza na Mamlaka ya Utangazaji ya Israel, mpango huo ulifichuliwa wakati wa kikao cha serikali ambacho Waziri wa Mambo ya Nje wa Marekani, Anthony Blinken alishiriki.

Shirika hilo la utangazaji limeongeza kuwa wajumbe wa serikali walikubaliana kwa kauli moja kuhusu umuhimu kujenga wa uzio huo wa usalama.

Ilibainisha kuwa Blinken alihoji mpango huo wa Israel baada ya kumalizika kwa vita hivyo na alijibiwa Israeli itaweka uzio huo na itachukua usimamizi wa usalama eneo la Ukanda wa Gaza.

Aidha, Wizara ya Ulinzi ya Syria ilitangaza jana kuwa jeshi la Israel limefanya mashambulizi katika eneo la mji mkuu wa Damascus na kusababisha hasara ndogo.

Wizara huyo ilisema tukio hilo lilitokea jana alfajiri na kujibiwa na vikosi vyake vya ulinzi wa anga kwa kurusha makombora dhidi ya ndege za uvamizi na kuzidungua.

Israel ilifanya shambulio la anga kutoka eneo la Golan upande Syria linayokaliwa kwa mabavu, ikilenga baadhi ya maeneo yaliyoko karibu na mji wa Damascus.

Kwa upande wake, mkurugenzi wa Shirika la Kutetea Haki za Binadamu la Syria, Rami Abdel Rahman, aliiambia AFP kwamba jeshi la anga la Israel lilishambulia kwa mabomu ngome za wanamgambo wa Hezbollah katika kitongoji cha Sayyida Zeinab, kusini mwa Damascus.

Aliongeza kuwa magari ya kubebea wagonjwa yalikimbilia eneo la tukio.

Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Damascus ulisitisha shughuli zake tangu Jumapili iliyopita baada ya kushambuliwa kwa bomu na ndege za Israel, kulingana na shirika la uangalizi la Syrian Observatory.

**BBC**



Mgombea wa upinzani Moise Katumbi, akihutubia mkutano wa kampeni katika mji wa Goma hivi karibuni. **PICHA: AFP**

# Kampeni uchaguzi DRC zaweka kambi mashariki

**KINSHASA,** DRC

KAMPENI za uchaguzi mkuu wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) zinazidi kuchanja mbuga na eneo la mashariki limekuwa kete muhimu kwa wagombea.

Miji ya Bukavu, Bunia, Butembo, Beni, Goma na Oicha imekuwa ikiwindwa na wagombea kutokana na kuwa na watu milioni 44 wana haki ya kupiga kura.

Uchaguzi huo utafanyika Desemba 20, wapigakura watamchagua rais atakayeongoza taifa hilo tajiri barani Afrika.

Mfanyabiashara tajiri Moise Katumbi, mmoja kati ya wagombea 23 wanaowania kiti cha urais, alikuwa wa kwanza kwenda mjini Goma, mji mkuu wa jimbo la Kivu Kaskazini kusaka kura.

Katumbi na wagombea wengine wa upinzani wamemtuhumu Rais Felix Tshisekedi kwa kushindwa kukabili changamoto za kiusalama kwa kulidhibiti kundi la waasi wa M23.

Kwa upande wa Rais Tshisekedi, ambaye anataka kuongoza kwa muhula wa pili wa miaka mitano, naye pia anatarajiwa kufanya kampeni eneo la mashariki ambapo ataanza mji wa Bunia katika mkoa wa Ituri Jummane ijayo.

Naye mshindi wa Tuzo la Nobeli, Dk. Denis Mukwege, alizindua kampeni zake Jumapili ya wiki iliyopita katika mji wa Bukavu alikozaliwa katika jimbo la Kivu Kusini.

Mgombea mwingine Martin Fayulu, anaendelea na kampeni zake kwa kufanya mikutano katika mji wa Beni ulioko Kivu kaskazini siku hiyo ya Jumanne.

**RFI**

# Burkina Faso, Mali, Niger zataka kuanzisha shirikisho

**BAMAKO,** MALI

MAWAZIRI wa mambo ya nje wa mataifa yanayotawaliwa kijeshi ya Burkina Faso, Mali na Niger wamependekeza kuunda shirikisho.

Hatua hiyo imeelezwa ni kama sehemu ya lengo la muda mrefu la kuunganisha mataifa hayo jirani ya Afrika Magharibi.

Katika mkutano huo walikubaliana, kuanzisha shirikisho hilo na kuliita Muungano wa Nchi za Sahel, wenye lengo la kuimarisha uhusiano wa karibu wa kiuchumi na ulinzi.

Katika taarifa yao ya pamoja baada ya mkutano huo wa siku mbili uliofanyika katika mji mkuu wa Bamako nchini Mali, mawaziri hao walizungumzia masuala ya amani, utulivu, kujenga diplomasia na maendeleo ya kiuchumi ili kutoa fursa ya kupatikana siasa imara katika mataifa yao.

Mali na Burkina Faso, zinazotawaliwa na viongozi wa kijeshi ambao walichukua mamlaka katika mapinduzi ya mwaka 2020 na 2022.

Nchi ya Niger kwa upande wake utawala wa kijeshi uliingia madarakani Julai mwaka huu kwa kumuondoa Rais Mohamed Bazoum.

**DW**

# Rais Rajoelina aidhinishwa kuongoza tena Madagascar

**ANTANANARIVO,** MADAGASCAR

MAHAKAMA Kuu ya Katiba nchini Madagascar imeidhinisha Rais Andriy Rajoelina ndiye mshindi wa uchaguzi uliofanyika Novemba 16.

Kulingana na mahakama hiyo, rais huyo wa sasa wa nchi hiyo ataendelea na nafasi yake baada ya kupata ushindi wa asilimia 58.96 ya kura zote zilizopigwa.

Mahakama hiyo imetupilia mbali kesi zilizokuwa zimewasilishwa kupinga ushindi wake.

Moja ya pingamizi zilizokuwa zimewasilishwa ilitoka kwa mpinzani wake wakili Siteny Randrianasoloniaiko.

Wagombea 10 kati ya 13 waliokuwa wamejiandikisha kuwania urais, waliususia uchaguzi huo ingawa majina yao tayari yalikuwa katika makaratasi ya kupigia kura.

MAKALA

# JE, KUWAJIBIKA NI UTAMADUNI WETU?



Na Magabilo Masambu

**Ukweli ni kwamba katika siasa za CCM kujiuzulu kwa Katibu Mkuu si jambo jipya. Aliyekuwa Katibu Mkuu wa CCM, Abdulrahman Kinana, amewahi kuwasilisha barua ya kujiuzulu mwaka 2018 kwa mwenyekiti wa chama wa wakati huo, Rais John Joseph Magufuli.**

KATIKA juma hili, pamekuwapo na habari mbalimbali zilizogonga vichwa vya habari katika vyombo vyetu vya habari nchini. Moja ya habari ni kuhusu kujiuzulu kwa Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Daniel Chongolo, ambaye alichukua nafasi hiyo Aprili 2021.

Taarifa za kujiuzulu kwake zilianza kusambaa kupitia barua iliyokuwa ikitembea katika mitandao ya kijamii siku kadhaa kabla ya mwenyekiti wa CCM na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan, kuthibitisha kuipokea katika kikao cha kawaida cha Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC), kilichofanyika jijini Dar es Salaam, Jumatano wiki hii.

Ukweli ni kwamba katika siasa za CCM kujiuzulu kwa Katibu Mkuu si jambo jipya. Aliyekuwa Katibu Mkuu wa CCM, Abdulrahman Kinana, amewahi kuwasilisha barua ya kujiuzulu mwaka 2018 kwa mwenyekiti wa chama wa wakati huo, Rais John Joseph Magufuli.

Tofauti kati ya Chongolo na Kinana zinaweza kuwa ni sababu za kujiuzulu, yaani kilichofanya wajiuzulu katika nyadhifa hiyo. Hata hivyo, mwenezi na msemaji wa chama hicho, Paul Makonda, hakuweka wazi hasa sababu zilizofanya Chongolo kujiuzulu japo katika barua yake kwenda kwa mwenyekiti, inaeleza kuwa ni kutokana na kuchafuliwa mitandaoni.

Pamoja na hayo yote, swali linasalia pale pale je, kuwajibika pale yanapotokea makosa fulani fulani katika utendaji wa vyama, serikalini au utumishi wa umma ni utamaduni wetu? Je, huwa tunafanya hivyo kwa maslahi ya umma au kunakuwapo na sababu nyinginezo ambazo huwa haziwekwi wazi?

Nasema hivi kwa sababu kuna baadhi ya watu au viongozi wamekuwa na tuhuma za waziwazi lakini kuchukua hatua kama ya Chongolo inakuwa msamiati, wakati mwingine waliowateua huchukua hatua ya kuwafuta kazi bila wao wenyewe kuwajibika.

Kiongozi anayejali maslahi ya umma na kulinda heshima yake, anatakiwa kuchukua uamuzi mara tu anapohusishwa na tuhuma zozote, lakini kwa nini kwa baadhi ya viongozi jambo hili linakuwa gumu sana? Je, wale wanaochukua uamuzi wa kufanya hivyo, wanaamua wenyewe au kuna msukumo wa kushinikizwa kufanya hivyo bila wao kwanza kuwa na wazo la kufanya hivyo na hasa hii miaka ya karibuni?

Katika awamu iliyopita ya uongozi wa nchi yetu, tulishuhudia mambo ya kuunga mkono juhudi, watu wakijiuzulu katika nafasi zao mbalimbali za vyama, halafu kesho unaona wamekwenda mahali fulani na wanateuliwa kuwa viongozi, nikawa najiuliza hivi huku ni kuwajibika ama ni kuandaa mazingira ya kutafuta nafasi zaidi au ilikuwa na maana gani hasa?

Ni kweli kwamba si kila anayefanya uamuzi wa kujiuzulu katika nafasi fulani, anaandaa mazingira ya kupata nafasi nyingine au ni msukumo utokao nje yake. Wako wanaofanya hivyo kwa kulinda heshima binafsi lakini na tasisi wanazoziongoza. Rais wa awamu ya pili, Mzee Ali Hassan Mwinyi, akiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, aliwahi kujiuzulu baada tu ya kutokea mauaji ya wazee mkoani Shinyanga, yaliyofanywa na watumishi wa wizara yake. Aliwajibika kwa niaba yao kama mkuu wa ofisi.

Nataka niamini kwamba Mzee Mwinyi, kama alivyofahamika na wengi Mzee Rukhsa, alifanya hivyo kulinda heshima ya ofisi na yake binafsi kama kiongozi lakini pia kuonyesha uwajibikaji wa kutowajibika sawasawa wakati matukio kama hayo yanatokea.

Yaani hapa ni sawa na ukiwa na mtoto mwizi, cha kwanza tunauliza kama ana wazazi. Kama wapo na mtoto akawa mwizi hata kama wizi huo kafundishwa na majirani au watoto wenzake, wa kwanza kulaumiwa ni mzazi kwa kutowajibika sawasawa. Yaani mzazi hawezi kujitetea kwamba hajamfundisha wizi. Ni kweli hujamfundisha lakini alishindwa kumdhibiti.

Aina ya uwajibikaji wa viongozi wetu unaleta shaka kwa sababu unaonekana kama si utamaduni uliyojengeka katika jamii yetu, ungekuwa utamaduni basi wako viongozi wengi ambao sasa hivi tunavyozungumza wangelikuwa wameachia ngazi na wako mtaani au wanafanya kilimo.

Mfano mdogo tu ni wale wote waliyotajwa katika ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) wasingesubiri kuchunguzwa wakiwa ofisini, wangeachia uchunguzi ukafanyika kwa uhuru na wakionekana hawana shida wanarudi kuliko kukomaa ofisini na wakati mwingine wanazuia uchunguzi kufanyika kwa ufanisi. Huwezi kumchunguza mtu kwa sababu kwa namna yoyote ile ataharibu uchunguzi. Swali je, kwa nini wako ofisini mpaka sasa? Kwa nini wasifuate mkondo wa Chongolo?

Mwisho, nakupongeza Chongolo kwa kuchukua hatua hiyo. Iwe ni hiari yako, msukumo kutoka nje, kwa maslahi ya chama na nchi yako haijalishi. Lakini kwa picha kubwa ya uwajibikaji umefanya jambo jema na hii haiwezi kuwa mwisho wa uongozi wako ndani ya chama na serikali.

Mzee Rukhsa alijiuzulu lakini baadaye akawa Rais wa nchi yetu piga moyo konde, pengine hatua uliyochukua itaonyesha njia kwa wale tunaotegemea wajiuzulu kutokana na tuhuma mbalimbali katika ofisi wanazoziongoza.

**0689157789**
**magabilomjalifu@gmail.com**
**Dar es Salaam-Tanzania**

BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# *Naomba tusahauliane 'Dear Ex'*



Na Adam Fungamwango

**Hii ni hatua ambayo wale wapenzi wawili kila mmoja anakuwa ameshaanza kugundua uzuri na ubaya wa mwenzake. Yaani kila mmoja ameshaanza kujua tabia halisi za mwenzake. Awali kila mtu alikuwa amezificha.**

KACHEZE unakocheza, kata simu tuko saiti, niondolee kasheshe, chondechonde, hala hala 'dear ex.' Unamrudia ex wako ama bora kufa? Bora kufa. Mrudiane ama bora kufa? Bora kufa."

Hiki ni kipande cha ngoma ya msanii wa kizazi kipya Mario 'Dear Ex.' Ameshakorofishana na kuachana na mpenzi wake wa zamani kwa sasa hana hamu naye tena. Anasema kurudiana naye, ni bora tu kufa.

Mwanamuziki wa dansi, Dk. Remmy Ongala, ameshawahi kuimba wimbo mmoja akizitaja hatua tatu za mapenzi. Ya kwanza ni tamu kama chungwa. Hapa ndipo Marijani Rajab alipoimba kuwa 'penye pengo huita kuna mwanya na kwenye chongo huona kuna kengeza.'

DDC Mlimani Park nao wakaimba 'mwenye mapenzi haoni, ingawa macho anayo.' Halafu wakaongeza, mtu chake apendacho hakina hila machoni, huridhika kuwa nacho japo hakina thamani.'

Hapa mtu kuambiwa chochote kile na mwenza wake akatekeleza. Hata watu wakija kumwambia kasoro za mpenzi wake hatoweza kuwaamini na kukubali.

Halafu inafuata hatua ya pili, ambayo Dk. Remmy alisema ni uchachu kama limao.

Hii ni hatua ambayo wale wapenzi wawili kila mmoja anakuwa ameshaanza kugundua uzuri na ubaya wa mwenzake. Yaani kila mmoja ameshaanza kujua tabia halisi za mwenzake. Awali kila mtu alikuwa amezificha.

Tabia ya kama kucha za paka au simba, hata ziingie ndani, lakini zitatoka tu.

Hatua hii kinachoendelea ni kila mmoja kujali zile faida za mwenzake, lakini anachofanya ni kuvumilia upungufu wa mwenzake kwa sababu hakuna binadamu ambayo hana kasoro duniani.

Hapa sasa mapenzi yataendelea kwa kila mmoja kama kuegemea na kuthamini mazuri ya mwenzake kama yatakuwa mengi kuliko upungufu.

Remmy amemalizia kwa kusema, mwisho wa mapenzi uchungu kama shubiri au kama pilipili.

Hapa sasa ndipo unapokutana na maneno kama yale ya Mario. Hapa kila mmoja amemchoka mwenzake. Kila mmoja atasema 'najuta kwa kutosikiliza maneno niliyoambiwa na watu mwanzo.'

Kila mmoja hapa anaona upungufu wa mwenzake kwa asilimia mia moja kwa sababu wameshachokana. Mapenzi hakuna tena. Pengo ni pengo na si mwanya tena, chongo ni chongo na wala si kengeza.

Kila mmoja anajuta kumfahamu mwenzake na lawama kibao wanatipiana. Hii ipo enzi na enzi na wala haitofutika. Ndiyo maana hata wasanii wa kizazi kipya wana nyimbo kibao zinazohusu wapenzi kuachana na kuziita 'Dear Ex.'

"Dear Ex, nimepata tetesi ya kwamba unisema ili nionekane si mwema, pengine una stresi maana umekonda mwepesi, kwangu ukimya si kilema ila chunga vya kusema maana niliubeba msalaba nikawa mimi ndiyo baba, nikajichanganua tujaze kibaba..."

Hii ni mistari na ngoma mpya tu ya Harmonize akimpa makavu laivu 'Dear Ex' wake, na watu tayari wameshaanza minong'ono kuwa wanamfahamu huyo shemeji yao wa zamani aliyepigwa na kitu hicho kizito.

"Eti ninywe sumu kisa wewe, uongo acha kujiongopea na ile tatoo niliyokuchora kifuani ni piko tu cha kuiongelea, huna jipya wewe kwanza umedoda, ukija baa hununui hata soda. Nimekutana na ex wangu kakonda mbwa yule, masela nimekutana na ex wangu kafubaa mbwa yule." Huu ni wimbo wa 'Dear ex' wa Mzee Wa Bwax, akimponda mpenzi wake wa zamani.

Miaka ya 1970, Patrick Balisidya alifyatua kibao akakiita 'Naomba Tusahauliane', kikiwa na maudhui haya haya ya maneno wanayoambiana watu walioachana kwa sasa wanajulikana sana kwa jina la 'Dear Ex.'

"Dadaaa, sikutegemea kusahauliana nawe kamwe kwa jinsi mimi nilivyokupenda, lakini nakiri ya kuwa tusahauliane. adaaa, mpenzi kwa heri japo katika majonzi yangu, huku nikitumanini kabisa kwamba utayajutia maisha yetu pamoja.

Dadaaa, kweli utengano wetu ni kitu kichungu lakini si kigeni katika maisha ya kila siku, tafsiri yako na yangu, zimegongana.

Neno hilo upendo na imani zetu zimetufanya tufarakane. Neno hili upendo na tabia zetu zimekuwa si sawa eli dada. Na hivi ndivyo inavyokuwa katika mapenzi dada. Aaa nadhani tulikosea kufanya pupa eli dada.

Aaaa ilibidi tujichunguze sana katika misimamo yetu dada. Katika jambo hili hatukufanya hivyo ole wetu ole wetu dada.

Baibai, baibai, baibai,baibai, baibai."

Ukiyasoma hayo mashairi ya wimbo huo yameandikwa kwa uchungu sana. Kikubwa anasema watu huingia kwenye mahusiano kwa msukumo na mapenzi, lakini wakati hawajasomama au kuchunguzana misimamo yao, tabia, mienendo na hii inasababisha kufarakana baadaye kila mmoja akija kugundua hawako sawa, hawaendi njia moja.

Haya ndiyo mapenzi, ni kizungumkuti, hayajawahi kumuacha salama binadamu yoyote aliyeishi kwenye sayari hii.

**Tuma meseji 0716 350534**

# HADITHI

CAROLINA, binti mrembo, aliyeumbwa akaumbika, mwenyewe anajiita Carry. Akifahamu fika jinsi alivyo mzuri na kubabaisha kila mwanaume anayekutana naye barabarani, anageuka kuwa mtu mwenye kiburi, jeuri, dharau na majivuno kwa watu. Atamsalimia yule tu aliyempenda kumsalimia. Ataongea na mtu atakayemchagua na si kila mtu. Anaweza kuziba hata pua akipita mtu ambaye yeye anaona si wa hadhi yake. Si mwanaume wala mwanamke. Jirani na anapoishi, kuna kijana mgeni asiyepungua miaka 25 hivi aliyehamia hivi karibu eneo la Kinondoni Moscow. Anaitwa James.

# Kafie Kwenu-22

Alikuwa kijana anayeishi maisha ya hali ya chini, akipanga chumba kimoja. Jicho lake naye liliona urembo wa Carry. Akaamua kujaribu. Kilichompata hatosahau maishani mwake. Fuatilia hadithi hii ya kusikitisha, kuhuzunisha, kufurahisha, kuburudisha na kufundisha kwa wakati mmoja.

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

WAKATI anatoa mkono, ghafla walisikia kitu kinaanguka chini na kubimbirika kikitoa mlio mkali.

Catty na dada yake walishtuka. Wakajiuliza ni kitu gani hicho.

Mtu pekee ambaye hakuwa ameshtuka ni James. Yeye alijua kitu gani anafanya, au anataka kufanya.

Upesi akainama chini na kuiokota. Hakuna yeyote kati ya wanawake wawili ndugu aliyekiona, au kujua nini kimeokotwa.

James alifungua kiganja chake cha mkono na kumuonyesha.

Ni kama alikuwa kwenye ndoto ambayo hajui kama ni mbaya au nzuri. Akapigwa na butwaa. Hakutegemea kukutana na kitu kama kile kwa muda ule. "Hivi ni kweli au naota?" Akajiuliza.

Akabaki amesimama kama mlingoti akimkodolea macho James.

"Naomba nikuvishe!" James aliongea kwa sauti ndogo, nyepesi na ya unyenyekevu.

"Lo, Mungu wangu, univishe nini James?" Catty aliuliza kwa mshangao huku ameshika kichwa.

Wakati huo, Carry alikuwa amekaa kwenye kochi, akiwa anashuhudia mchezo, macho yakiwa yamemtoka. Akaonekana kama mtu ambaye kama anatabasamu, halafu anarudi kwenye hali yake ya kawaida.

"Pete."

"Uko siriasi kweli James?"

"Niko siriasi Catty."

Catty aliendelea kuwa kama mtu aliyechanganyikiwa hivi.

"Si ulisema unaye..." Catty, akakumbuka maongezi ya mwisho aliyoongea na James mara ya mwisho alipokuja

"Eee jamani uje, basi umlete hata huyo wifi yetu tuje kumuona." James akacheka, halafu akamjibu.

"Nimekwambia ninaye ninayetaka kumuoa. Ila siwezi kuja naye hapa hadi nimuoe."

"Ndiyo ninaye. Ni wewe."

"Ulivyonijibu vile ilikuwa ni mimi?"

"Ndiyo, na ndiyo maana nilikwambia siwezi kuja naye hapa kwa sababu wewe ulikuwa hapa hapa!"

Catty alianza kumuelewa James, ingawa miguu iliendelea kucheza kwa mchanganyiko wa mashangao, wasiwasi na furaha pia.

"James, kwa nini mimi?" Catty akauliza swali ambalo James alikuwa akilihitaji muda wote.

"Ulinijali na kunithamini wakati sina kitu. Fukara wa kutupwa. Hohehahe na mtu aliyekuwa akidharauliwa na watu wengi.

Ukanipa aina fulani na furaha ambayo niliwaza kuwa siku nilipata mke nahitaji awe kama wewe. Ulinisaidia, kunijali kwa shida na raha bila kutarajia malipo ya kitu chochote kutoka kwangu kwenye maisha yako yote. Ulifanya hivyo kwa ajili ya utu, roho nzuri na wema. Ulinichukua wakati nilipougua. Sikuwa na pesa, nilihitaji matibabu na chakula pia kwa sababu sikuwa na uwezo wa kufanya kazi tena. Nilihitaji msaada na kutunzwa pia. Hakuna aliyefanya hivyo zaidi ya wewe.

Nilikula hapa mara tatu kila siku zaidi kiasi cha miezi mwezi na nusu hivi. Ulinipa pesa za matibabu. Niliposhinda kesi ya mirathi na kufanikiwa kuingizwa kwenye urithi wa marehemu kaka yangu nilijiuliza sana kuhusu kutafuta mke wa kuona sasa ili kujenga familia. Kwa akili yangu tu nikaona kuna mtu anafaa kuwa mke. Ni wewe Catty. Lakini nikawa najiuliza, atakubali?" Maneno yalivyokuwa yakimtoka James ilikuwa kana kwamba anaomboleza hivi.

"Mama yangu Farida akanijia kwenye ndoto, akaniambia hataki nioe mwanamke mwingine ila ni wewe uliyenijali na kunisaidia wakati wa shida. Nikamuuliza, mama atakubali? Akaniambia mwanangu huyo ndiye mkeo, nenda kamwambie, ghafla nikaamka."

"Sawa, kwa hiyo unahitaji nini kwangu?"

"Ulinijali wakati watu wote wanidharau. Naomba unipende sasa wakati watu wanaanza kuniheshimu. Katika maisha yangu yaliyobaki, sitokuwa na raha na amani kama hutokuwa karibu yangu. Hata utajiri nilionao haitokuwa na maana kwa sababu nataka niutumie na mtu ambaye anilifadhili, kunijali na kuniheshimu. Naomba nikuvishe pete hii, nikuoe uwe mke wangu."

Catty akakumbuka pia maneno ya dada yake Carry.

"Unaweza kumshawishi James akawa na wewe. Niko radhi kabisa James akuchukue wewe ili asituponyoke. Mimi kwangu imeshindikana, lakini wewe kwa sababu ni rafiki yake na mengi umemfanyia na amekuwa akikubali, anaweza kukubali uwe mpenzi wake akuoe!"

"Mmmh! Yeye alikuwa anakuhitaji wewe! Hakuna hata siku moja James aliyowahi kuniambia nakupenda hata kwa bahati mbaya pamoja na kuwa ni rafiki yake sana,japo lingefuta machozi yetu." Akakumbuka maongezi yao siku kadhaa nyuma. Na leo imekuwa hivyo.

Catty akauza shingo akamtazama dada yake Carry. Akaona ishara ikimwambia,"fanya hivyo."

Akasogea taratibu kwa James, akapeleka mkono wake kushoto, James akamvisha pete kidoleni.

Carry akapiga kelele za furaha kiasi cha kuwashangaza James na Catty wenyewe.

"James, machozi yananitoka kwa furaha, mchukue mdogo wangu, inawezekana yote yalipangwa na Mungu. Mimi nimejifunza vitu vingi kupitia kwako. Naahidi sitofanya hivi kwa mtu yoyote, binadamu hujifunza kutokana na makosa. Mchukue mdogo wangu utakuwa umetusitiri sana. Nisingejisamehe kama tungekukosa na kuchukua mwanamke mwingine." Maneno yalimtoka Carry huku akilia.

"Usijali Carry. Haya yote yaliyotokea yanawakuta binadamu ili ajifunze. Nadhani hutorudia tena na mimi naahidi kuwa shemeji yako mzuri. Tutakwenda wote na dada yako kuishi kwangu Ununio na mtafanya kazi kwenye makampuni yetu." Akamkumbatia Carry ambaye alikuwa anatokwa na machozi ya furaha.

James akarudi kwa Catty."Naahidi nitakuwa mwema na mume bora kwako. Kwanza kabisa nimeshafanya mpango wa kununua eneo lile lote ambalo nilikuwa naishi kwenye kile kijumba ili nijenge nyumba kubwa nzuri. Ni eneo ambalo siwezi kuliacha kwa sababu ya kumbukumbu yangu. Nitapangisha, lakini nitaacha vyumba viwili wazi kwa ajili ya kuja kumpumzika huku kama vile mtu anakwenda kijiji wakati wa likizo."

Catty akamkumbatia James kimahaba kwa mara ya kwanza huku machozi yakimtoka.

"Nilistahili hili. Mungu amelipa maombi yetu. Hata sisi tumepitia maisha magumu na ya tabu, baada ya wazazi wetu kufariki. Kwa bahati nzuri tulisomeshwa kidogo na shangazi, kiasi cha kupata kazi kwenye hoteli za kitalii. Leo nakwenda kuwa mke wa mtu tajiri anayeendesha makampuni ya baba yake. Katika maisha yangu, sikutegemea kitu kama hiki. Naahidi nitakuwa mke mwema. Nitafanya zaidi ya kile ambacho ulikiona kutoka kwangu."

Waliendelea kukumbatiana, kila mtu akiwa na hamu na mwenzake. Kwa kuwa walifanya hivyo kwa mara ya kwanza kama wapenzi rasmi.

Kila mmoja alikuwa na hisia kali kwa mwenzake. James aligeuka nyuma akakutana na tabasamu la Carry akionyesha kufurahia mdogo wake na James tayari ni wapenzi rasmi. Akamuonyesha ishara Catty ageuka kumuona dada yake. Akageuka kumtazama, wakapeana ishara ya ushindi. Carry akaanza kupiga vigelegele.

**MWISHO**




**"Ulinijali na kunithamini wakati sina kitu. Fukara wa kutupwa. Hohehahe na mtu aliyekuwa akidharauliwa na watu wengi. Ukanipa aina fulani na furaha ambayo niliwaza kuwa siku nilipata mke nahitaji awe kama wewe. Ulinisaidia, kunijali kwa shida na raha bila kutarajia malipo ya kitu chochote kutoka kwangu kwenye maisha yako yote.**

# Vanessa, Rotimi wafurahia maisha wakiwa baharini

MWANAMUZIKI mkongwe wa Bongo Fleva, Vanessa Mdee na mume wake Rotimi, wiki hii wameonyesha jeuri ya fedha baada ya kukodi boti maalumu kwa ajili ya kufurahia maisha.

Mdee kupitia ukurasa wake wa Instagram aliweka video fupi akiwa na Rotimi ambaye alikuwa anasherehekea siku yake ya kuzaliwa.

Wawili hao walionekana wakiwa ndani ya boti wakivinjari baharini huku kila mmoja akiwa anakunywa kinywaji chake anachokipenda.

Hata hivyo, Vanessa alifichua kwamba pamoja na bata hilo hakugusa kinywaji chochote chenye kileo kwa sababu ameacha kutumia miaka minne iliyopita.





# USALAMA WA DIAMOND MASHAKANI?

USALAMA wa staa wa muziki wa Bongo Fleva uko mashakani? Ndivyo watu wengi wanajiuliza kufuatia tukio la hivi karibuni la mwanamuziki huyo kuporwa kofia mbele ya walinzi wake.

Tukio hilo lilitokea mjini Dodoma, wakati alipotoka katika duka moja la kuuza simu katika harakati zake za kutangaza tamasha burudani la Wasafi.

Kulingana na video ambayo iliyosambaa mitandaoni Diamond alionekana akiwa na rundo la walinzi wake wakipita katikati ya umati wa watu, ndipo mtu mmoja alipompora kofia na kutokomea nayo.

Diamond alionekana kukerwa na aliamuru watu wake kuitafuta kwa sababu ndiyo anaitegemea kupanda nayo jukwaani.

Kofia hiyo hatimaye ilipatikana na kurudishwa kwa Diamond baada ya kukutwa kwa waendesha pikipiki maarufu bodaboda wakiishangaa.

Baadhi ya watu waliotoa maoni yao, walidai usalama wa mwanamuziki huyo uko mashakani kutokana na walinzi wake hawana weledi ya kazi yao.

Wengi walihoji ikiwa kofia hiyo imeporwa hadharani, hivyo walinzi hao wanaweza kukabiliana na matukio ya ghafla kumlinda mwanamuziki huyo?

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

**PHILLIPS AWANIWA NEWCASTLE**

KLABU ya Juventus inajiandaa kumnunua kiungo wa Manchester City, Kalvin Phillips mwenye umri wa miaka 27. (***Mail***)

**IVAN KUBAKI**

KOCHA wa Brentford, Thomas Frank anatarajia mshambuliaji wa England, Ivan Toney mwenye umri wa miaka 27 atasalia katika klabu hiyo baada ya uhamisho wa Januari. (***Standard***)

**MINTEH KUREJESHWA**

KLABU ya Newcastle inafikiria kumrejesha winga wa Gambia, Yankuba Minteh mwenye umri wa miaka 19 kutoka katika kipindi chake cha mkopo na Feyenoord ili kusaidia kupunguza matatizo yao ya majeraha. (***Telegraph***)

**GUIRASSY ATAKIWA MAN**

KLABU za Manchester United na Newcastle United zinataka kumsajili mshambuliaji wa Stuttgart mwenye umri wa miaka 27 kutoka Guinea, Serhou Guirassy katika uhamisho wa pauni milioni 15. (***Guardian)***

**SPURS KUNUNUA WACHEZAJI**

ANGE Postecoglou amesema Tottenham Hotspur huenda ikalazimika kununua mchezaji Januari baada ya wachezaji kadhaa wa klabu hiyo kuwa majeruhi au kushiriki michuano ya Kombe la Mataifa ya Afrika (Afcon). (***Sky Sports***)

**VLAHOVIC KUONGEZA**

MSHAMBULIAJI wa Juventus, Mserbia Dusan Vlahovic mwenye umri wa miaka 23 ameanza mazungumzo ya mkataba mpya na klabu hiyo na kuleta pigo kwa Manchester United na Arsenal ambazo zinamwania. (***Gazzetta delo Sport***)

**EDOUARD ATAKIWA PALACE**

KLABU ya West Ham inachunguza uwezekano wa kumnunua mshambuliaji wa Crystal Palace, Odsonne Edouard mwenye umri wa miaka 25 Januari wakati ambapo kiungo wa Hispania, Pablo Fornals mwenye miaka 27 akitazamiwa kuondoka. (***Football Transfers***)

**BAKAYOKO AWINDWA**

KLABU za Tottenham Hotspur na Brentford zinawania kumsajili winga wa PSV raia wa Ubelgiji, Johan Bakayoko mwenye umri wa miaka 20 Januari. (Football Insider) Liverpool wanapania kumleta kiungo wa kati wa Nice na Ufaransa Khephren Thuram, 22, Anfield. (***Fichajes***)

**BOBB KUONGEZA MKATABA**

KLABU ya Manchester City inakaribia kufikia makubaliano ya mkataba mpya na mshambuliaji wa Norway, Oscar Bobb mwenye umri wa miaka 20. (***90 min***)

**BARCA HAITALIA**

BARCELONA haitalipa ada ya euro milioni 50 iliyowekwa kwenye kifungu cha kutolewa katika mkataba mpya wa mshambuliaji wa Athletic Bilbao, Nico Williams, katika hatua ambayo inampa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21 fursa ya kujiunga na klabu zingine msimu ujao. (***Mundo Deportivo)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# RONALDO AKEJELIWA KWA JINA LA MESSI

**RIYADH,** Saudi Arabia

CRISTIANO Ronaldo alitoka nje ya uwanja huku akizomewa kwa kelele za "Messi, Messi, Messi" kutoka kwa mashabiki wenye furaha wa Al Hilal ambao walishuhudia timu yao ikiichapa Al Nassr na nyota huyo wa Ureno mabao 3-0 kwenye mchezo wa dabi ya jiji la Riyadh, Ijumaa.

**Mshindi huyo mara tano wa Ballon d'Or aliondoka uwanjani kichwa chini baada ya Aleksandar Mitrovic kufunga mara mbili baada ya Mserbia mwenzake, Sergej Milinkovic-Savic kufunga bao la kwanza kwa Al Hilal, lakini Ronaldo bado anabakia kuzingatiwa katika soka la Saudi Arabia.**

Wakati mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 38 akipasha misuli

**●●●Ni baada ya kupoteza mchezo wao dhidi ya Al Hilal na mashabiki wa....**

kabla ya mchezo huo, kulikuwa na shangwe kutoka kwa mashabiki wake, ambao wengi wao walikuwa wamevaa jezi yenye namba 7 migongoni mwao.

Katika mechi 14 zilizopita za msimu wa ligi, mshambuliaji huyo wa zamani wa Real Madrid na Manchester United alikuwa amefunga mabao 15 na hivyo kuisaidia Al Nassr ambayo pia ina nyota wa zamani wa Liverpool, Sadio Mané, kiungo wa kati wa Croatia, Marcelo Brozovic na mchezaji wa zamani wa Manchester United, Alex Telles - sasa ipo nafasi ya pili kwenye ligi nyuma ya Al Hilal.

"Cristiano ni mfano kwa kila mtu, mfano ambao Al Nassr wana bahati kuwa nao," alisema kocha wa Al Nassr Luis Castro kuhusu Ronaldo baada ya mchezo huo.

"Yeye ni mfano wa ukali, tamaa na nidhamu. Watu wengi wanataka kuwa kama Cristiano Ronaldo, lakini wachache wanataka kufanya kazi kama Cristiano Ronaldo. Ikiwa unataka kitu lazima utoe kila kitu ili kukipata."

Ronaldo alijaribu kila kitu katika mchezo huo, alipiga shuti kali lililotinga wavuni lakini likakataliwa kwa madai kuwa ameotea.

Kichapo cha dabi ya Ijumaa kiliiacha Al Nassr alama saba nyuma ya Al Hilal inayoongoza ligi baada ya raundi 15.

Ronaldo anaweza kuwa na kazi ngumu ya kuisaidia timu yake kushinda taji la 10, lakini.



# NEWCASTLE YAJITOSA KWA PHILLIPS

**NEWCASTLE,** England

KLABU ya Newcastle United inapanga kuimarisha nia yao ya kutaka kumnunua kiungo wa kati wa Manchester City, Kalvin Phillips wakati wa dirisha la usajili la Januari, imeripoti ESPN.

Magpies wanapanga kuongeza nguvu kwenye safu yao ya kiungo baada ya mchezaji aliyesajiliwa majira ya joto, Sandro Tonali kufungiwa kwa makosa ya kujihusisha na kamari.

Nia ya klabu hiyo kwa Phillips ni kumsajili Phillips na kwamba Man City wanaweza kumruhusu kuondoka Januari.

Kutokana na sheria ya haki sawa kwa manunuzi inamaanisha kwamba, Newcastle ingependelea kumchukua Phillips kwa mkopo.

Man City watakuwa tayari kuidhinisha hili, lakini ikiwa tu mpango kama huo unakuja na chaguo la kumnunua.

Ingawa klabu kadhaa kutoka England na Ulaya - ikiwamo Aston Villa, Liverpool, Tottenham Hotspur, West Ham United, Borussia Dortmund na Juventus zimeonesha nia ya kutaka kumsajili Phillips mwenye umri wa miaka 27 hivi karibuni.

Phillips kwa sasa hayumo katika mipango ya muda mrefu ya Kocha wa Man City, Pep Guardiola.

Ingawa ameweka shida zake za majeraha katika msimu wake wa kwanza kwenye Uwanja wa Etihad nyuma yake, Phillips amecheza dakika 215 tu kwa Man City msimu huu na ameanza mchezo mmoja tu ambao walipoteza 1-0 kutoka kwa Newcastle katika mzunguko wa tatu wa Kombe la Carabao.

Licha ya muda wake wa kucheza mechi kuwa mdogo katika ngazi ya klabu, Phillips alikuwa na nafasi yake katika kikosi cha England cha kocha, Gareth Southgate.

# Klopp akiri kuzuia wachezaji kuondoka

**LIVERPOOL,** England

KOCHA wa Liverpool, Jurgen Klopp amekiri kuwa alilazimika kuzuia kutolewa kwa mkopo kwa mlinda mlango, Caoimhin Kelleher majira ya joto ili kutimiza sheria za usajili wa kikosi hicho.



Kelleher alijiunga na Liverpool miaka nane iliyopita na alipanda daraja katika akademi kabla ya kupandishwa daraja hadi kwenye kikosi cha wakubwa mwaka wa 2019. Tangu wakati huo, amekuwa akiitumikia kama kipa mbadala na Klopp.

Akiwa amekwama nyuma ya Alisson kama kipa namba moja, Kelleher mwenye umri wa miaka 25 amecheza mechi 27 pekee za soka ya klabu katika maisha yake yote ya wakubwa, na mechi kumi zaidi kwa Jamhuri ya Ireland kwa jina lake.

Katika kutafuta dakika zaidi za kucheza, Kelleher alikuwa tayari kuondoka Liverpool kwa mkopo msimu huu wa joto, lakini Klopp alilazimika kuzuia uhamisho huo kwa sababu ya thamani ya mlinda mlango huyo.

"Tulikuwa na majadiliano katika msimu wa joto kwa hakika kuhusu kuendelea lakini mradi tu hatuna suluhu hatuwezi kuwakopesha wachezaji," alisema Klopp.

"Yeye ni mzaliwa wa nyumbani na jukumu la kwanza ni kufanya vizuri zaidi kwa Liverpool na lazima tuone jinsi ya kutatua.

"Sasa ni wazi kwake, ni hali ambayo hakutaka kuwa nayo, lakini, ni wazi, kwa namna fulani ndiyo kwa sababu unataka fursa, unataka kucheza, sasa atapata michezo michache bila shaka. Ninamwamini."

Kelleher anatazamiwa kucheza mechi kadhaa baada ya jeraha la Alisson na atacheza mechi ya sita tu ya Ligi Kuu wakati Fulham itakapoelekea Anfield leo Jumapili.

"Tunamwona kila siku mazoezini, ni kipaji cha kipekee," Klopp alisema kuhusu Kelleher.

"Labda hatutaji jina mara nyingi vya kutosha, lakini John Achterberg (kocha wa makipa wa Liverpool) aliniambia tangu siku ya kwanza nilipokuwa ndani kwamba huyu atakuwa mtoto wetu wa nyumbani ambaye atafanikiwa."

# Guirassy kutua Ligi Kuu England

**LONDON,** England

WAWAKILISHI wa Serhou Guirassy wanazidi kujiamini kuwa mshambuliaji Guirassy atajiunga na timu ya Ligi Kuu ya England wakati wa dirisha la uhamisho la Januari, kwa mujibu wa 90min.

Guirassy amekuwa na kiwango bora msimu wa 2023/24 baada ya kufunga mabao 16 katika mechi 11 kwenye mashindano yote hadi sasa kwa Stuttgart.

Idadi yake ya mabao 15 kwenye Bundesliga imezidiwa na Harry Kane pekee wa Bayern Munich, ambaye ametikisa nyavu mara 18 tangu kuhamia huko akitokea Tottenham Hotspur msimu wa joto.

90min iliripoti Oktoba kwamba mkataba wa Guirassy na Stuttgart una kipengele cha kutolewa chenye thamani ya takriban pauni milioni 15.2, wakati maskauti kutoka

Bournemouth, Brentford, Crystal Palace na West Ham United walikuwa wamesafiri kwenda Ujerumani kumwangalia mapema msimu huu.

Klabu hizo zimepewa fursa ya kumsajili Guirassy na vimeendelea kufuatilia uchezaji wake, ingawa pia amekuwa akihusishwa na kuhamia Manchester United katika siku za hivi karibuni.

90min inaelewa kuwa United pamoja na Arsenal, Everton, Newcastle, Tottenham na Wolves - zote zimewasiliana na wawakilishi wake kuhusiana na hali ya Guirassy na kambi yake naamini kuwa klabu zote hizo zina nia ya kiwango fulani, ingawa hakuna ofa iliyotolewa.

Uhamisho wowote unaowezekana katikati ya msimu unaweza kutatanishwa na uwezekano wa Guirassy kuhusika na Guinea katika Kombe la Mataifa ya Afrika, ambalo litaanza Januari 13.

Nchi zinazoshindana zinaruhusiwa kuwaita wachezaji kwenye kambi ya mazoezi wiki mbili kabla ya michuano hiyo.



# KATWILA: TUNA NAFASI YA KUFANYA VIZURI

**Na Saada Akida**

LICHA ya kushika mkia wakiwa nafasi ya 16 kwenye msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Kocha Mkuu wa Mtibwa Sugar, Zuberi Katwila, amesema bado wana nafasi ya kufanya vizuri kwenye Ligi Kuu na wataanza kuonyesha hilo kwenye mchezo wao unaofuata dhidi ya Namungo FC.

Mtibwa Sugar inaendelea kusuasua baada ya kupoteza michezo saba, ikishinda mmoja na sare mbili katika michezo 10 ambayo tayari wameshacheza katika ligi hiyo ikikusanya alama tano huku ikiburuza mkia.

**Wakata miwa hao wa Manunngu, Tuliani wa takuwa na kibarua De semba 7 ugenini dhidi ya Namungo FC kwenye Uwanja wa Majaliwa, Ruangwa mkoani Lindi.**

Akizungumza na Nipashe jana, Katwila alisema wana hali mbaya baada ya kutofanya vizuri katika michezo 10 ya mwanzo wa msimu na sasa wanapambana kufanyia kazi makosa yaliyopo ili kutojirudia kwenye mechi zijazo wakianzia na Namungo FC.

Alisema hali ni mbaya na kwa sasa wapo kwenye mapambano makali, wanalazimika kutumia akili kubwa na nguvu kufanya kazi sana na kutokata tamaa kwa matokeo ya nyuma.

"Ligi ina ushindani hakuna cha kupata matokeo nyumbani wala ugenini, kikubwa ni kuendelea kupambana hadi dakika ya mwisho, nitajitahidi kujenga akili za wachezaji wasione huu ndio mwisho wao, bado kuna nafasi kubwa ya kutoka hapa tulipo na kupanda kwenye nafasi ya juu ya msimamo," alisema Katwila.

Aliongeza kuwa nafasi iliyopo kwa sasa inamuumiza kila mmoja na wanatakiwa wachezaji wapambane ili kujiondoa kwenye hiyo nafasi na kupanda nafasi za juu kujiweka katika nafasi nzuri kwenye msimamo.

Alisisitiza kuwa anafanyia kazi mapungufu ya kikosi chao na anaimani kuanzia mechi ijayo watafanya vizuri kwa kusaka alama muhimu katika mchezo huo watakaocheza ugenini.



Golikipa wa Timu ya Kipela, Hamis Shaibu, akidaka mpira huku akizongwa na mchezaji wa Kitunda, Ayub Michael, katika mchezo wa kirafiki uliopigwa Uwanja wa Shule ya Msingi Kitunda jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Kundemba FC mambo magumu Z'bar

**Na Hawa Abdallah,**
ZANZIBAR

MAMBO yameendelea kuwa magumu kwa Timu ya Kundemba FC baada ya kupokera vichapo vitatu mfululizo katika michezo ya Ligi Kuu ya Zanzibar.

Kundemba jana ilichezea tena kichapo cha mabao 2-1 dhidi ya Mabingwa wa tetezi wa Ligi hiyo KMKM SC mchezo uliochezwa katika Uwanja wa Mau A ukiwa ni mzunguko wa 13 wa Ligi Kuu ya Zanzibar.

Kundemba FC huo unakuwa mchezo wake wa sita kupoteza katika michezo 13 iliyocheza mpaka sasa kwenye ligi hiyo.

Akizungumza na Nipashe jana, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Ali Vuai, alitupia lawama kwa mwamuzi wa Ligi Kuu kwa kutotekeleza vyema sheria 17 zinazowaongoza.

Alisema timu yake inacheza vizuri tangu kuanza kwa Ligi Kuu ya Zanzibar lakini waamuzi ndio wanaochangia kuwarejesha nyuma kwa kutotoa uamuzi sahihi hasa kwa upande wa timu yao.

Alidai kuwa hujuma hizo zinazofanywa na waamuzi hao zinapelekea hata wachezaji kuvunjika moyo kutokana na kushindwa kufanyiwa haki jitihada zao wanazozionesha kwa timu yao katika dakika 90.

"Timu yetu inacheza vizuri sana katika timu zote za Ligi Kuu ya Zanzibar hata idadi ya magoli tunayofungwa yanakuwa "2-1 au 1-0" hatujawahi kufungwa magoli matatu tangu tuanze ligi lakini waamuzi hawa tunasema ndio wanatuhujumu kwa kutufungisha kwa makusudi, wanaonekana kama wanapewa maagizo watufungishe," alisema Vuai.

Aidha, alisema iwapo waamuzi hao watachezesha kwa haki michezo yao miwili iliyobaki ya kukamilisha mzunguko wa kwanza basi wanauhakika wa kupata alama tatu kwa kila mchezo.

Hata hivyo aliwaomba viongozi wa Bodi ya Ligi Zanzibar kuwafuatilia kwa karibu waamuzi wanaochezesha Ligi Kuu ya Zanzibar ili iweze kuwa na mvuto na kila timu iweze kushinda kwa jitihada zake.

## Simba, Yanga mambo magumu

INATOKA UK. 24

ushindi kwenye mechi yao ya Kundi B, kwani ilitawala karibuni muda mwingi mwa mchezo, hasa kipindi cha kwanza lakini wachezaji wake walionekana kutokuwa makini kuweka mipira ndani ya nyavu.

Kama Jena Baleke na Saido Ntibazonkiza wangekuwa makini wangeweza kuipatia bao Simba sekunde ya 55 tu baada ya mechi kuanza, kutokana na kazi nzuri ya Kibu Denis aliyemtoka beki wa kushoto Lesego Keredilwe na kumimina majaro ambayo iliwapita mbele yao.

Dakika tatu baadaye, Kibu tena alifanya kazi nzuri baada ya kumtoka tena Keredilwe lakini washambuliaji wa Simba walichelewa kuingia kwenye eneo la hatari na krosi yake nzuri ikaokolewa na mabeki wa Jwaneng.

Beleke alifanya jaribio lingine dakika tano baadaye alipopenyezewa pasi na Willy Onana, lakini wakati anataka kuunganisha kwa mguu wake wa kushoto badala ya kupiga mpira akapiga mguu wa beki wa kati Thabo Lenanyane na kumpa nafasi kipa Goitseone Phoko kuukamata mpira kirahisi.

Kipa huyo alifanya kazi ya ziada dakika ya nane alipodaka mpira wa kichwa kilichopigwa na Sadio Kanoute uliotokana na kona ya Saido.

Dakika moja baadaye ilikuwa zamu ya kipa wa Simba, Ayoub Lakred, alipoiokoa timu yake isifungwe bao kutokana na shambulizi kali la kushtukiza.

Lilikuwa ni shambulizi la kwanza kwa Jwaneng Galaxy likifanywa dakika ya tisa, wakati straika wao hatari Daniel Msendami alipoupata mpira mrefu na kuanza kuwatoka mabeki wa Simba mmoja baada ya mwingine, kabla ya kutaka kuuweka wavuni, lakini Lakred aliruka na kucheza mpira kwa mguu na kuwa kona tasa.

Baleke alipata nafasi nyingine ya kuandika bao dakika ya 24, lakini akiwa ana kwa ana na kipa Phoko, shuti lake lilidakwa.

Kocha, Mualgeria Abdelhak Benchikha aliyekuwa benchi kwa mara ya kwanza akimrithi Mbrazil Roberto Oliveira, alifanya mabadiliko ya wachezaji kipindi cha pili kwa kumtoa Kanoute, Kibu, Saido na Onana, na kuwaingiza Clatous Chama, Mzamiru Yassin, Luis Miquissone na Moses Phiri, lakini bado walishindwa kupata dawa ya kuipenye ngome ya Jwaneng Galaxy na kupata bao.

Nafasi pekee kubwa ambayo wanachama na mashabiki wa Simba wataiota ni ile ya dakika ya 90, ambapo shuti la mguu wa kushoto la Chama lilikwenda kugonga mlingoti wa pembeni kwa chini na kurudi uwanjani, ukamkuta Baleke ambaye alipiga shuti kubwa juu ya lango.

Kwa matokeo hayo, Simba wanakusanya pointi mbili katika michezo miwili waliyoicheza na sasa wanasubiri mchezo unaofuata dhidi ya Wydad Casablanca kabla ya kuanza michezo ya marudiano.

# Michezo

Jumapili Desemba 3, 2023

Nipashe

UKURASA 22



**Newcastle yajitosa kwa Phillips**



# Simba, Yanga mambo magumu CAF

## Ingawa kila timu bado ina nafasi, lakini kwa matokeo haya wamejiweka katika.....

**Na Adam Fungamwango**

WAWAKILISHI wa Tanzania kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika hatua ya makundi, Simba na Yanga jana zilijiweka katika mazingira magumu kwenye makundi yao kusonga mbele japo bado wana nafasi ya kufanya hivyo licha licha ya matokeo ya jana kwenye michezo yao ya ligi hiyo.

Wakati Simba ikitoka sare bila kufungana na wenyeji wao Jwaneng Galaxy kwenye Uwanja wa Obed Itani Chilume nchini Botswana mechi iliyochezwa mapema, saa 10 jioni, Yanga ililazimishwa sare ya bao 1-1 na Mabingwa Watetezi, Al Ahly ya Misri, mechi ikichezwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, saa 1:00 usiku.

Bao la dakika ya 90 lililowekwa wavuni na Kiungo mshambuliaji raia wa Ivory Coast, Pacome Zouzoua, liliiokoa Yanga kupata kipigo cha pili katika Kundi D dhidi ya Mabingwa Watetezi wa michuano hiyo, Al Ahly ya Misri.

Pacome alifunga bao hilo akiwa ndani ya eneo la hatari kwa shuti huku akizingirwa na mabeki wa Al Ahly wakati akipokea pasi ya Kennedy Musonda aliyeingia kipindi cha pili kuchukua nafasi ya Clement Mzize.

Bao hilo la Pacome lilikuja dakika ya 89 baada ya wageni Al Ahly kutangulia kwa bao la dakika ya 87 la nyota wa Afrika Kusini, Percy Tau.

Tau aliunganisha kwa kichwa mpira uliookolewa kizembe na Bakari Mwamnyeto, huku kipa Diarra akiwa ametoka langoni kutokana na krosi ya Karim Fouad aliyeambaa na mpira wingi ya kushoto kabla ya kupiga krosi hiyo iliyowashinda mabeki wa Yanga.

Yanga ilianza mechi hiyo kwa kasi, ikifanya mashambulizi mfululizo yaliyoiwezesha kupata kona tatu ndani ya dakika kumi za mwanzo, lakini zote ziliondoshwa na mabeki wa Al Ahly.

Mzize nusura aipatie Yanga bao dakika ya tisa kama si kazi kubwa iliyofanywa na kipa Mohamed El Shenawy akiwa amebaki na kipa huyo na mpira mguuni huku akisumbuliwa na mabeki wawili waliokuwa pembeni yake alijikuta akipiga mpira nje huku Stephane Aziz Ki akiwa kwenye nafasi nzuri ya kufunga kama angepewa pasi hiyo.

Iliwachukua Al Ahly dakika 13 kufika kwa mara ya kwanza katika lango la Yanga, wakati, Emam Ashour alipowatoka mabeki wa Yanga na kuachia shuti kali lakini kipa Djigui Diarra aliyekaa langoni kwa mara ya kwanza akitoka kwenye majeruhi alilidaka.

Yanga ilipata pigo dakika ya 33 ya mchezo baada ya Joyce Lomalisa kuumia na kushindwa kuendelea na mchezo na Kocha Mkuu wa Yanga, Miguel Gamondi akalazimika kumuingiza Nickson Kibabage kuchukua nafasi yake.

Kwa matokeo ya jana, kwa upande wa Yanga wapo katika nafasi ya mwisho kwenye msimamo wa kundi D linaloongozwa na Al Ahly wenye pointi nne baada ya ushindi dhidi ya Medeama ya Ghana waliyoifunga mabao 3-0 na sare ya jana dhidi Yanga, CR Belouizdad ya Algeria wanashika nafasi ya pili wakiwa na pointi tatu sawa na Medeama, Yanga wanashika mkia wakiwa na pointi moja.

Jijini Francistown, Simba itabidi ijilaumu yenyewe kwa kushindwa kutoka bila

INAENDELEA UK. 23

9 770856 541002 >

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042